**RAIS** Samia aahidi ushirikiano zaidi Tanzania, Malawi katika biashara

UKURASA 2



**MAJALIWA** atoa mbinu vijana kunasa ajira za lugha Kiswahili

UKURASA 17


Ukurasa 13
Watanzania tuwe 'serious' kwa mambo 'serious'!
BUFE
IJUMAA JULAI 7, 2023
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA
Hifadhi Mkomazi na faru adimu mweusi anayelipiwa kwa mkataba
Ukurasa 12
WIKI YA 77 NA BIASHARA
Rais Samia awafungua macho wana-SADC kilimo kinavyohamia sokoni
Na Mwandishi Wetu

UKURASA 11


# Nipashe

Ijumaa Julai 7, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581364

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


# Kaka ashtakiwa kubaka dada yake kwa miaka mitano

**ASOMEWA** shtaka lingine la kumwambukiza VVU kwa makusudi, akosa dhamana... *Endelea ukurasa 7*



Rais Samia Suluhu Hassan akiweka shada la maua kwenye kaburi la Rais wa Kwanza wa Malawi na Baba wa Taifa hilo, Hayati Dk. Kamuzu Banda katika Makumbusho ya Kamuzu, Lilongwe jana. **PICHA: IKULU**



## Bei ya sukari yapaa dukani, bodi yakana kuhusika nayo

UKURASA 2

UKURASA WA 18

## WASIOJULIKANA WACHINJA WANANDOA

WANANDOA wakazi wa Kitongoji cha Mwagimagi, Kijiji cha Shilebela, Kata ya Ulewe, Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga...

UKURASA WA 5

## SIMBACHAWENE AWACHARUKIA WATUMISHI WAPENDA RUSHWA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, amekemea...



## Jaji Mkuu asema amesikia mtandaoni, hayana tija

UKURASA 3



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akikata utepe kuzindua rasmi madarasa na ofisi za Shule ya Msingi Muyama wilayani Buhigwe, mkoani Kigoma juzi, yaliyokarabatiwa na Benki ya Biashara Tanzania (TCB). Wengine ni Mkurugenzi Mkuu wa TCB, Sabasaba Moshingi (kushoto), Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, CP Thobias Andengenye (wa tatu kushoto) na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Joyce Ndalichako (wa pili kulia). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

**MICHEZO** WAKONGWE SIMBA, YANGA WATAKA WACHEZAJI WAZAWA KUJITAMBUA UK. 24

**KATUNI** UK. 6

# Samia aahidi ushirikiano zaidi Tanzania na Malawi kiuchumi

**Na Jenifer Gilla**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema Tanzania itaendelea kudumisha ushirikiano wa kiuchumi na nchi ya Malawi kwa kufanya kazi kwa karibu katika biashara na uzalishaji mali ili kuboresha ustawi wa wananchi na kukuza uchumi wa mataifa hayo.

Alitoa ahadi hiyo jana alipohutubia katika sherehe za miaka 59 ya Uhuru wa nchi hiyo zilizofanyika katika Ukumbi wa Kimataifa wa Bingu, mjini Lilongwe.

Rais Samia pia alimhakikishia Rais wa nchi hiyo, Lazarus Chakwera, kuwa Tanzania itaendelea kuwa mshirika wa kutegemewa kimkakati na kamwe haitokuwa kikwazo cha ukuaji wa maendeleo ya nchi hiyo.

"Tanzania haitokuwa kikwazo kwa njia ya Malawi kuelekea ustawi wa kiuchumi kwani tunaona ustawi wa Malawi ni kama ustawi wetu. Tanzania itaendelea kuheshimu wajibu wetu na kusaidia ukuaji wenu," alisema Rais Samia.

Alisema tangu Rais wa nchi hiyo aje Tanzania mwezi Oktoba 2020, uhusiano wa serikali na watu wa nchi hizo umezidi kuimarika. Wataendelea kufanya kazi kwa karibu ili kustawisha ushirikiano wa kibiashara.

Rais Samia alisema ili kufikia malengo hayo, nchi hizo zinapaswa kushughulikia changamoto za kibiashara ambazo jumuiya zao zinakabiliwa nazo ikiwamo kuwezesha na kurahisisha usafirishaji wa bidhaa na huduma. "Bahati nzuri masuala haya yalijadiliwa katika Tume ya Pamoja ya Kudumu kati ya nchi zetu mwaka jana. Nimeambiwa kuwa majadiliano yalikuwa ya kirafiki, pande zote mbili ziliridhia na kukubaliana kufanya kazi pamoja katika kutatua changamoto.

"Niko hapa kusherehekea nanyi ili kuelezea kuridhishwa kwetu na uhusiano bora uliopo kati ya nchi zetu na kurudisha mshikamano na dhamira ya kuendelea kushirikiana nanyi kwa ustawi wa nchi zetu mbili na watu wetu," alisema.

Rais Samia alimpongeza Rais Chakwera kwa kuadhimisha siku hiyo muhimu na uhusiano bora walioudumisha kimataifa.




Waziri wa Nishati, January Makamba, akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kufikiwa kwa kina cha maji cha kuzalisha umeme katika Bwawa la Nyerere jijini Dar es Salaam jana na kikao cha mawaziri sita Tanzania na Zambia kuhusu ujenzi wa bomba la mafuta kutoka Tanzania kwenda Zambia kitakachofanyika leo chini ya uenyekiti wake. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bei ya sukari yapanda Dar

**Na Jenifer Gilla**

BEI ya jumla na rejareja ya sukari imepanda mkoani Dar es Salaam huku wafanyabiashara wakidai ongezeko hilo la bei linatokana na uzalishaji kupungua viwandani.

Bodi ya Sukari Tanzania (SBT) imekanusha madai ya kupungua kwa uzalishaji wa sukari viwandani na haioni sababu za kupandisha bei ya bidhaa hiyo.

Katika udadisi wake maeneo mbalimbali mkoani hapa yakiwamo Tabata na Gongo la Mboto wilayani Ilala, Makumbusho na Manzese wilayani Kinondoni na Tandika wilayani Temeke, mwandishi amebaini bei ya sukari kwa mauzo ya jumla imefikia Sh. 69,000 mwezi huu kutoka Sh. 64,000 mwezi Mei kwa mfuko wa kilo 25 na kwa rejareja sasa inauzwa Sh. 3,000 kutoka Sh. 2,800 kwa kilo.

Wakati bei ya bidhaa hiyo ikipanda sokoni, bei elekezi ya bidhaa hiyo kwa Mkoa wa Dar es Salaam iliyotolewa mwaka 2021, yaani miaka miwili iliyopita, ni Sh. 2,600 kwa kilo.

Baadhi ya wafanyabiashara walidai bidhaa hiyo ilianza kuadimika na hivyo kupanda bei tangu Mei. Nao wakalazimika kuongeza bei wapate faida.

Mfanyabiashara mwenye duka la vyakula anavyoviuza kwa bei ya rejareja huko Tabata jijini, Celina Damas, alidai kwa sasa ananunua mfuko wa kilo 25 wa sukari kwa Sh. 69,000 kutoka Sh. 64,000 iliyokuwa bei ya bidhaa hiyo Mei mwaka huu. Anadai bei ilianza kupaa mwezi uliopita.

Kwa kuzingatia bei ya anakonunulia, mfanyabiashara alisema analazimika kuuza kilo moja kwa Sh. 3,000 kutoka Sh. 2,800 ili kufidia gharama iliyoongezeka. Alipopandisha bei, wateja walikimbia, lakini wameanza kurejea.

Tuna mwezi sasa bidhaa hii imepanda sasa. Tunaingia mwezi wa pili huu (Julai). Mwezi Juni hali ilikuwa mbaya kwa maana ulikuwa unaweza kukaa hadi siku mbili hupati sukari kwenye maduka ya jumla, ukiipata unakuta imeongezeka Sh. 500," alidai.

Mfanyabiashara mwenye dula la jumla anayefanya shughuli zake Makumbusho, Twalibu Kajame, alidai walipata taarifa (bila kutaja aliyewapatia taarifa) kwamba kuanzia mwezi huu wa Julai kutakuwa na ongezeko la bidhaa hiyo sokoni.

Alisema kuwa awali walikuwa wananunua mfuko wa kilo 25 kwa Sh. 63,000 na kuuza kwa Sh. 64,000 lakini kwa sasa umefikia Sh. 68,000, hivyo wanalazimika kuuza kwa Sh. 69,000 ili kufidia gharama.

Alisema kupanda kwa bei kumezua malalamiko kwa wateja hasa pale wanapokwenda kufuata sukari na kukuta bei tofauti wakati mwingine wanashindwa kabisa kununua.

Alisema siku mbili zilizopita hali ilikuwa mbaya zaidi tofauti na sasa na kutaja bidhaa nyingine ambazo zimepanda ni pamoja na maziwa ya kopo yaliyokuwa yanauzwa Sh. 23,000 kwa sasa ni Sh. 30,000, sigara paketi moja imepanda kutoka Sh. 4,300 hadi Sh. 5,500.

Mfanyabiashara wa chakula katika Soko la Mwenge wilayani Kinondoni, Judith Salema, alisema bei ya sukari ikipanda zaidi, itawalazimu nao wapandishe gharama ya chakula ili kufidia.

"Machungu tumeshaanza kuyaona ingawa sio sana, kama sukari ikiendelea kupanda itabidi na sisi tupandishe vyakula vinavyotumia sukari kama uji, chai, tambi, maandazi, vitumbua na kalimati," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Sukari Tanzania, Kenneth Bengesi, katika ufafanuzi wake kwa mwandishi kuhusu suala hilo wiki hii, alisema hakuna sababu bei ya bidhaa hiyo kupanda kwa sasa kwa kuwa hata msimu wa viwanda kusimamisha uzalishaji umeshapita.

"Kwa kawaida viwanda vinasimama uzalishaji mwezi Machi hadi Juni. Hata hivyo, (kipindi hicho) huwa tunaingiza sukari kutoka nje ili kufidia. Hakuna sababu yoyote ya sukari kupanda bei," alisema.

Kenneth aliahidi kufuatilia suala hilo kujua sababu za wafanyabiashara kupandisha bei na wao kulishughulikia ili bei zirudi kama zilivyokuwa mwanzo.

Katika hotuba yake wakati wa Bunge la Bajeti lililopita, alipowasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka huu wa fedha, Waziri wa Wizara hiyo, Hussein Bashe, alisema wameanza kuchukua hatua mbalimbali ili kuongeza uzalishaji wa sukari ikiwamo kuongeza upatikanaji wa mbegu bora na kuanzisha kilimo cha umwagiliaji.

Alisema lengo ni kuhakikisha uzalishaji wa miwa katika mwaka 2023/24 unafikia tani 4,500,000 ambazo zitazalisha tani 465,000 za sukari kama inavyotarajiwa.

Alisema hali hiyo itasaidia kupunguza nakisi ya sukari kutoka nje kwa kiwango kilichopo sasa cha tani 30,000 ili kufikia mwaka 2025 kusiwapo uagizaji wa sukari kutoka nje.

Uzalishaji wa miwa unatarajiwa kufikia tani 7,000,000 ambazo zitazalisha tani 700,000 za sukari kufikia mwaka 2025, ambao ndiyo ukomo wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Juni 1999-2025.

# Bwawa la Nyerere lajaa, uzalishaji umeme kuanza

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI wa Nishati, January Makamba, amesema kazi ya ujazaji wa maji katika mradi wa kufua umeme kwa maji wa Mwalimu Nyerere umefikia kiwango kinachotosheleza kuzalisha umeme.

January alibainisha hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari katika ofisi za wizara hiyo mkoani Dar es Salaam.

"Kama mnavyofahamu kumekuwa na hofu kubwa kwamba maji yatajaa ya kuwezesha kuzalisha umeme? Habari njema ni kwamba ndani ya msimu mmoja, tumefanikiwa kujaza maji kiwango cha kutosheleza kuzalisha umeme.

"Kina cha bwawa lote lile ni mita 184 kutoka usawa wa bahari. Kina kinachotakiwa kufikiwa ili uanze kuzalisha umeme ni mita 163 kutoka usawa wa bahari. Siku ya jana (juzi) tumefikia mita 163.61, maana yake ni kwamba tumefika na kupita kinachotakiwa kwa ajili ya kuzalisha umeme.

"Maana yake ni kwamba kuanzia sasa, maji yote yanayojaa pale ni ya ziada na kama tungekuwa tumemaliza ufungaji wa mitambo, tungeanza kuzungusha hata leo (jana), lakini kazi ya ufungaji mitambo hiyo inaendelea," alisema.

Waziri huyo alisema ujazo wa bwawa hilo ni mita za ujazo bilioni 30 na kwamba mpaka jana (juzi), maji yaliyoingia ndani ni mita za ujazo bilioni 13 sawa na asilimia 43.

"Kwa hiyo, tuko vizuri kwenye kina na tuko vizuri kwenye ujazo na tuko vizuri kwenye ratiba," alisema na kubainisha wanatarajia Februari mwakani kuanza majaribio ya kuzungusha mitambo hiyo.

Alisema wanatarajia mpaka Juni mwakani wataanza kutoa umeme katika bwawa hilo na kuingiza katika Gridi ya Taifa.

"Na juzi nilisafiri kwenda China kuangalia mitambo yetu ya kuzalisha umeme itakayofungwa ili kuhakikisha ratiba ya uzalishaji inafikiwa. Na kifaa cha mwisho kabisa kutoka China chenye mitambo kitaondoka China Novemba 30 mwaka huu na kutuwezesha kuwa ndani ya ratiba," alisema.

Pia alisema kuwa leo mawaziri sita wa Wizara za Nishati na Mambo ya Ndani wa Tanzania na Zambia wanakutana jijini Dar es Salaam kwa ajili ya kujadili usalama wa bomba la mafuta kutoka Kigamboni mpaka Zambia na kupokea taarifa ya ujenzi wa bomba jipya la gesi na ujenzi wa bomba jipya la mafuta.

**HABARI KITAIFA**

# Somo dawa za kulevya kuingizwa kwenye mitaala

**Na Maulid Mmbaga**

KAMISHNA Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), Aretas Lyimo, amesema kuna mchakato unaendelea ili kuingiza somo la elimu ya dawa za kulevya kwenye mitaala kufundishwa kuanzia shule ya msingi mpaka vyuo ili kuepusha kundi kubwa la Watanzania kuingia kwenye dawa za kulevya.

Alisema hayo jana akiwa katika banda la mamlaka hiyo, katika Maonesho ya 47 ya Biashara ya Kimataifa, jijini Dar es Salaam, huku akieleza kuwa watu wengi wanajihusisha na dawa za kulevya kutokana na kukosa uelewa wa kutosha kuhusu madhara yake.

"Tumeandaa mwongozo wa ufundishaji ambao kupitia Wizara ya Elimu na wadau wetu mbalimbali wanafunzi watafundishwa juu ya uelewa wa dawa za kulevya jinsi ya kuepukana nazo na madhara yake kwa ujumla, hii yote ni kuhakikisha tunakomesha tatizo hili," alisema Lyimo.

Pia wanashirikiana na Wizara ya Kilimo kufanya utafiti na operesheni nchi nzima ili kubaini mikoa iliyokithiri kwa kujihusisha na kilimo cha dawa za kulevya ikiwamo bangi na mirungi kuwawezesha wahusika kufanya shughuli zingine na kuachana na kilimo hicho.

"Iko mikoa inayoongoza sana kwa kilimo cha bangi ikiwamo Arusha, Mara, Morogoro, Ruvuma na Iringa, lakini inayolima mirungi kama Tanga na Kilimanjaro na kote tunaenda kutoa elimu, lakini Wizara ya Kilimo itafanya utafiti ili kuja na mazao mbadala ili waachane na kilimo hicho," alisema Lyimo.

Alibainisha kuwa changamoto wanayokutana nayo ni jamii haijachukua jukumu la kupambana na dawa za kulevya ikiwamo kuelimisha watu athari na ubaya wa dawa hizo na kwamba wazazi wengi hawachukui jukumu hilo na kulinda watoto wao.

Pia, alisema endapo wazazi na jamii kwa ujumla ingechukua jukumu la kuwalinda watoto wao kutojiingiza kwenye namna yoyote na dawa za kulevya tatizo hilo anaamini lisinge kuwapo.

Aliwataka viongozi wa kimila, kidini, vijiji na vitongoji hadi wa ngazi za juu na jamii kwa ujumla, kuwa kila mmoja kwa nafasi yake angekuwa anakemea jambo hilo na kuhakikisha sehemu yoyote linapotokea wanachukua hatua kukemea athari za dawa hizo kwa jamii lisingekuwa kubwa kiasi hicho.

"Hata kwenye mitaa kuna vijiwe vya watumiaji na wauzaji wa dawa za kulevya na jamii inawajua, lakini haichukui hatua kwa kutoa taarifa au kuwakamata, kwa hiyo hili la jamii kutojihusisha na kukemea dawa hizo ndilo linalokuza tatizo kubwa nchini, niwaombe kila mtu kwa nafasi yake ahakikishe anakemea dawa za kulevya," alisisitiza Lyimo.




Rais mstaafu Dk. Jakaya Kikwete akimsalimia Ofisa Msimamizi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Shaga Gagunda, alipotembelea na kupata nafasi ya kusalimiana na maofisa wa mamlaka hiyo wanaoshiriki katika kliniki ya biashara wakati wa Maonyesho ya 47 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam katika viwanja vya Sabasaba, barabara ya Kilwa jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Kikwete avipa jukumu vyuo vikuu utafiti kuinua uchumi

**Na Restuta James**

RAIS mstaafu wa awamu ya nne, Dk. Jakaya Kikwete, amezipa taasisi za elimu changamoto ya kufanya utafiti wenye majibu ya kubadilisha uchumi na sekta zote, akibainisha kuwa mageuzi yanayoendelea duniani yamesababishwa na vyuo vikuu.

Akizungumza jana baada ya kutembelea Maonesho ya 47 ya Biashara ya Kimataifa, maarufu Sabasaba, yanayoendelea Dar es Salaam, Kikwete alisema uvumbuzi wa utafiti huo ndio unaweza kuelekeza matumizi sahihi ya rasilimali za taifa kwa manufaa ya watu wengi.

"Tunategemea vyuo vyetu vifanye uvumbuzi kwa sababu maendeleo yote unayoyakuta huko duniani, yametoka kwenye vyuo, wote unaowaona huko wakubwa (wafanyabiashara wakubwa), wametoka kwenye vyuo," alisema.

Kikwete alisema vyuo vina nafasi ya kuhakikisha vinazalisha rasilimali watu yenye sifa stahiki ili kuendeleza na kukuza sekta zote zikiwamo za uchumi.

Alisema: "Shule zetu kuanzia msingi, sekondari, vyuo vya ufundi na vyuo vikuu vikifanya vizuri, tutapata rasilimali watu yenye kiwango cha juu. Ukipata wenye kiwango cha juu ndio mambo yenu mengi yatakuwa yanakwenda vizuri.

"Katika viwanda mtapata watu wanafanya kazi vizuri, kwenye kilimo mtapata wazalishaji wazuri, kwenye huduma mtapata za kiwango cha juu.

"Ukipata rasilimali watu ya kiwango cha juu, uchumi wa nchi unakua. Ukipata uvumbuzi wa kuwezesha matumizi ya rasilimali za taifa, uchumi unakua na kazi hiyo inaendelea kufanyika lakini hatujafika mwisho. Jitihada zaidi ziendelee," alihimiza.

Alisema maonesho hayo ni fursa kwa Watanzania kuonesha fursa za kibiashara na kiuwekezaji zilizopo nchini na kuwakutanisha wafanyabiashara wa ndani na wanaotoka mataifa mbalimbali.

Kikwete alisema wajasiriamali wanapaswa kuyatumia maonesho hayo kujitangaza kwa kuwa yana nafasi ya kuwakutanisha na masoko makubwa.

Alisema wapo wafanyabiashara kutoka mataifa mengine wanaotafuta sehemu za kuwekeza na wengine wanatafuta bidhaa kutoka Tanzania kwenda nchi zao.

# Jaji Mkuu asema amesikia mazungumzo mitandaoni

**Na Kulwa Mzee**

JAJI Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma, amesema ameyasikia yanayozungumzwa katika mitandao ya kijamii, akidai hayana tija.

Kiongozi huyo wa mahakama pia amewataka mawakili wapya kupambana na changamoto ya ukosefu wa ajira za kudumu nchini kwa kuona na kuibua fursa zinazotokana na mabadiliko ya teknolojia.

Pia amewataka mawakili wazione fursa zitakazopatikana katika soko huria la Afrika mapema badala ya kusubiri lianze ndipo waanze kulaumu na kuona wameingiliwa katika soko.

Prof. Juma aliyasema hayo jana wakati wa sherehe ya kuwapokea na kuwakubali mawakili wapya 195 kuwa mawakili wa kujitegemea.

Alisema mawakili hao 195 waliokubaliwa na kula kiapo, wanafanya idadi ya mawakili nchini kuwa 11,637. Hafla hiyo ya kuwapokea na kuwakubali mawakili ni ya 68 tangu kuanzishwa mwaka 1986.

"Kuna changamoto ya ajira za kudumu, taasisi hazitoi nafasi. Tukitoa mafunzo ya sheria tuhakikishe masomo yetu yawe ya kuwawezesha mawakili kupata fursa. Kuna mabadiliko makubwa na teknolojia tunapaswa kuyaelewa.

"Mabadiliko yanasababishwa na sayansi ya teknolojia. Mfumo huo umeondoa ajira, taasisi zilizokuwa zinatoa ajira kwa mawakili hazitoi tena, kazi hizo zinafanywa na ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

"Mawakili na wanasheria mjiweke katika hali ya kusoma fursa, muwe na miwani ya kuona fursa karne ya 21. Ninaona bado hamjaona fursa katika miradi mikubwa, kama mradi wa SGR," alisema Jaji Mkuu.

Alisema katika mikutano ya majaji wakuu wa Afrika wanazungumzia zaidi maeneo mapya ya fursa, wanazungumzia teknolojia, soko huria na nafasi ya mahakama itakuwaje.

"Sisi Watanzania bado tuko nyuma, wenzetu wanaona fursa lakini sisi kwa kuwa tunavaa miwani ya kizamani hatuzioni hizo fursa.

"Mawakili wa Tanzania hilo soko huria litakaposhika kasi, mko tayari au mtakuwa watu wa kulaumu kuona mnaingiliwa katika soko.

"Kuna mazungumzo ninayasikia katika mitandao hayana tija. Ninawaomba tuvae miwani ya karne ya 21. Tuangalie fursa zinazotokana na Soko Huria la Afrika," alisema Jaji Mkuu.

Jaji Mkuu amepewa mamlaka ya Sheria ya Mawakili Sura ya 341 toleo la mwaka 2019 kifungu cha 8(3) kuwakubali mawakili wapya.

Aliwafahamisha mawakili hao kuwa baada tu ya kula kiapo kila mmoja ni ofisa wa mahakama, wananchi wanategemea wawe na sifa nzuri, waadilifu na wakweli.

Kumekuwa na ukosoaji kuhusu kiongozi huyo kuendelea kubaki katika ofisi ya Jaji Mkuu wa Tanzania, hata kufunguliwa kesi ya kikatiba kupinga kuongezwa muda wa kuendelea kuwa madarakani.

KCBL KILIMANJARO CO-OPERATIVE BANK LIMITED
Together, Transforming Lives

**TANGAZO**

TUNAPENDA KUWAARIFU WENYEVITI NA WAJUMBE WA BODI WA VYAMA, MAKAMPUNI/TAASISI NA WANAHISA WOTE BINAFSI, KUWA MKUTANO MKUU WA ISHIRINI NA SITA (26) WA MWAKA WA WANAHISA WA BENKI YA USHIRIKA YA KILIMANJARO (KCBL), UTAFANYIKA SIKU YA IJUMAA, TAREHE 28 JULAI, 2023 KWENYE UKUMBI KURINGE SOCIAL HALL (BARABARA YA ARUSHA), MOSHI KUANZIA SAA TATU (3:00) ASUBUHI.

TUNAPENDA KUWAKUMBUSHA KUWA KILA CHAMA/TAASISI/KAMPUNI ITUME MJUMBE MMOJA TU, NA MWANAHISA BINAFSI ANAYO NAFASI YA KUHUDHURIA BINAFSI AU KUWAKILISHWA KWA MUJIBU WA MASHARTI YA BENKI.

KARIBUNI SANA.

**Godfrey J. Ng'urah**
**Katibu-Bodi ya Wakurugenzi**
**Tarehe: 05/07/2023**

SIKU YA KISWAHILI DUNIANI

# Jukwaa muhimu kujadili maendeleo lugha ya Kiswahili




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza katika ufunguzi wa Siku ya Kiswahili Duniani jijini Zanzibar jana. **PICHA: OWM**

**Na Richard Mtambi**

MAADHIMISHO ya Pili ya Siku ya Kiswahili Duniani (MASIKIDU), yanafanyika duniani kote Julai 7, 2023. Kwa hapa Tanzania yanafanyika Visiwani Zanzibar. Maadhimisho haya yanatokana na uamuzi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) wa Novemba, 2021 kuwa tarehe 7 Julai ya kila mwaka kuwe na Maadhimisho ya Siku ya Kiswahili Duniani.

Uamuzi huo ulitolewa wakati wa Mkutano wa 41 wa Nchi Wanachama wa Shirika hilo uliofanyika jijini Paris, Ufaransa.

Hatua hiyo inakifanya Kiswahili kuwa lugha ya kwanza ya Kiafrika kutambuliwa na kupewa siku yake maalumu ya kuadhimishwa.

Maadhimisho ya Siku ya Kiswahili Duniani 2023, kwa hapa nchini, yameandaliwa na Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) na Baraza la Kiswahili la Zanzibar (BAKIZA), chini ya usimamizi wa Wizara zenye dhamana ya utamaduni: Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ya Zanzibar.

Aidha, Maadhimisho haya yameandaliwa kwa kushirikiana na taasisi na idara zinazojihusisha na lugha ya Kiswahili na wadau wa lugha hiyo kwa ujumla. Vilevile, Maadhimisho haya yamefanikiwa kutokana na michango ya washirika mbalimbali wanaounga mkono jitihada za kukiendeleza.

Yanafanyika kwa mara ya pili, baada ya uamuzi huo wa UNESCO wa Novemba 2021, maadhimisho ya kwanza yalifanyika Julai 7, 2022 ambapo Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) liliandaa Mwongozo wa Maadhimisho ya Siku ya Kiswahili Duniani ambao ulisambazwa katika Balozi za Tanzania na kutumiwa na Balozi hizo katika kuadhimisha siku hiyo.

Maadhimisho ya mwaka huu nchini, yalianza kwa mbio za masafa za Kiswahili zilizofanyika jijini Arusha, Julai 1, 2023. Mgeni rasmi katika mbio hizo alikuwa Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Hamis Mwinjuma. Malengo ya mbio hizo yalikuwa ni kuleta ari na mwamko kwa Tanzania, Afrika na Duniani kote ili kuyapa hadhi, kuchochea na kuendeleza juhudi za kutangaza utalii, ambazo zilianzishwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, kupitia filamu aliyoianzisha ya Royal Tour.

Fauka ya hayo, mbio hizo zimekuwa na umuhimu wake kwa kuwaleta watu kwa pamoja kutoka sehemu mbalimbali duniani. Mbio hizo pia zimewasaidia washiriki kuimarisha afya ya akili na mwili, ikizingatiwa kuwa katika zama hizi watu wengi wanakabiliwa na magonjwa mbalimbali yasiyo ya kuambukiza kutokana na tabia bwete.

Aidha, mbio hizo zimetoa fursa mbalimbali kama kushiriki katika ubidhaishaji wa Kiswahili miongoni mwa washiriki na taifa kwa ujumla.

Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kupitia BAKITA imefanikiwa kuanzisha mbio hizo kwa kushirikiana na African Sports Agency (ASA) pamoja na wadau wengine. Zimepangwa kufanyika kila mwaka wakati wa maadhimisho haya mikoa tofauti ya Tanzania.

Kabla ya kufikia kilele chake leo, wadau wa Kiswahili walishiriki katika matukio mbalimbali yanayohusu maendeleo ya lugha ya Kiswahili Duniani. Tarehe 4 Julai, 2023, BAKITA kwa kushirikiana na BAKIZA waliandaa Jukwaa la Wahariri, Kikwajuni Zanzibar. Wahariri na wadau wengine wa Kiswahili walijadiliana mada ya 'Nafasi ya Wahariri Wakuu katika Matumizi ya Kiswahili Sanifu katika Vyombo vya Habari'. Aidha, tarehe 5 Julai, 2023 BAKITA na BAKIZA waliandaa mjadala mpana 'Kiswahili ni Nyenzo ya Ukombozi wa Fikra kwa Maendeleo ya Kiuchumi Barani Afrika.'

Pia, tarehe 6 Julai, kulikuwa na matembezi katika Skuli ya Sekondari ya Dk. Ali Mohamed Shein. Baada ya matembezi hayo kulikuwa na ufunguzi rasmi wa maadhimisho utakaofanyika katika ukumbi wa Chuo cha Polisi cha Zanzibar, Bomani Zanzibar. Kilele cha Madhimisho ya Pili ya Siku ya Kiswahili Duniani 2023 yanafanyika katika Ukumbi wa Chuo cha Polisi cha Zanzibar, Bomani Zanzibar leo. Maadhimisho haya yatahitimishwa kwa tukio la 'Usiku wa Taarabu' utakaofanyika katika Ukumbi wa Chuo cha Polisi cha Zanzibar, Bomani.

Maadhimisho haya yanafanyika katika kipindi ambacho BAKITA linatekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Kubidhaisha Kiswahili (2022/23 - 2031/32). Mkakati huu umeandaliwa na Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) na Baraza la Kiswahili la Zanzibar (BAKIZA), chini ya usimamizi wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ya Zanzibar. Mkakati huu ulizinduliwa rasmi na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Philip Isdor Mpango, tarehe 7 Julai, 2022 wakati wa Maadhimisho ya Kwanza ya Siku ya Kiswahili. Maeneo ya kipaumbele yanayoshughulikiwa katika utekelezaji wa mkakati huu ni pamoja na uuzaji wa taaluma za Kiswahili, ukuzaji na uimarishaji wa miundombinu ya kufundishia na kujifunzia Kiswahili, uuzaji wa machapisho ya Kiswahili, uuzaji wa rasilimaliwatu na uuzaji wa huduma mbalimbali za Kiswahili kama vile tafsiri, ukalimani, uhariri, ufundishaji wa Kiswahili kwa wageni na makundi mengine yanayohitaji, uandishi, utangazaji na ukuzaji wa sanaa ya Tanzania.

Katika kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Kubidhaisha Kiswahili, BAKITA limeendesha mafunzo ya kufundisha Kiswahili kwa wageni kwa Watanzania wanaoishi katika nchi mbalimbali duniani pamoja na kuwafundisha Kiswahili baadhi ya wananchi wa nchi hizo waliotamani kujifunza lugha hii. Miongoni mwa nchi zilizotembelewa na wataalamu wa BAKITA kwa ajili ya mafunzo hayo ni Malawi (Novemba, 2022), Burundi (Desemba, 2022) na Nigeria (Mei 2023). Nchi nyingine zilizopatiwa mafunzo hayo ni Falme za Kiarabu za Abu Dhabi na Dubai, Italia, Uholanzi, Zimbabwe na Rwanda (Juni, 2023).

Lengo kuu la mafunzo hayo ni kuwajengea uwezo Watanzania wanaoishi katika nchi hizo ili waweze kufundisha Kiswahili kama lugha ya kigeni kupitia vituo vilivyoanzishwa na balozi za Tanzania katika kutekeleza agizo la Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.) alilolitoa katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 11 Februari, 2021. Waziri Mkuu alizigiza balozi zote za Tanzania zilizoko katika mataifa mbalimbali zianzishe vituo vya kujifunzia lugha ya Kiswahili kwa wageni ili itumike kujenga diplomasia ya uchumi na Watanzania waweze kuajiriwa katika nchi hizo.

Aidha, BAKITA linaendelea kutekeleza maelekezo ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Philip Mpango aliyoyatoa tarehe 7 Julai, 2022 wakati wa Maadhimisho ya Kwanza ya Siku ya Kiswahili Duniani. Miongoni mwa maelekezo hayo yalikuwa ni kuhakikisha kuwa nyaraka za mawasiliano za Wizara na Idara zake ziandikwe kwa lugha ya Kiswahili na kwamba mikutano, warsha, semina, mijadala na umma na dhifa ziendeshwe kwa Kiswahili. Vilevile,

Makamu wa Rais aliagiza kuwa taarifa za miradi na mikataba inayohusu wananchi ni lazima iwe kwa lugha ya Kiswahili na isiwe kwa lugha za kigeni pekee na pia aliagiza kuwa Sheria na kanuni ambazo bado hazijatafsiriwa kwa Kiswahili, zitafsiriwe na Wizara na Taasisi zinazosimamia Sheria na kanuni hizo, kwa kushirikiana na Mabaraza ya Kiswahili (BAKITA na BAKIZA), watalaamu wengine wa Kiswahili na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Tangu kutolewa kwa maelekezo BAKITA limeshirikiana na wizara na taasisi mbalimbali zilizo chini ya wizara hizo kutafsiri Sheria, kanuni, miongozo, mipango na mikakati mbalimbali. Miongoni mwa Ofisi na Wizara zilizotafsiri nyaraka zake na wataalamu wa BAKITA ni Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ofisi ya Makamu wa Rais - Muungano na Mazingira, Ofisi ya Waziri Mkuu - Idara ya Menejimenti ya Maafa na Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu.

Aidha, wataalamu wa BAKITA wameshiriki kutafsiri nyaraka za Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo na taasisi zake, Wizara ya Maliasili na Utalii - Idara ya Misitu na Nyuki, Wizara ya Maliasili na Utalii - TANAPA, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, Wizara ya Afya, Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Madini na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. BAKITA linatasfiri nyaraka hizi ili wananchi waelewe kila jambo muhimu kwa ustawi wa maisha yao kama ambavyo iliagizwa na Makamu wa Rais, Mhe. Dk. Philip Isdor Mpango.

Watendaji Wakuu wa Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) na Baraza la Kiswahili la Zanzibar (BAKIZA) pamoja na wafanyakazi wote wa Mabaraza haya wanaahidi kuyafanyia kazi maelekezo, maazimio, maoni na mapendekezo yote yatakayotolewa katika Maadhimisho haya ya 2023. Aidha, Mabaraza haya mawili yatatoa taarifa zaidi ya ushughulikiaji wa maelekezo, maazimio, maoni na mapendekezo mbalimbali katika vyombo vya habari na kwa maandishi rasmi kwa wahusika. Vilevile, taarifa zaidi za ushughulikiaji wake zitatolewa katika Maadhimisho ya Tatu ya Siku ya Kiswahili Duniani, mwaka 2024.

Ni matarajio ya wadau wote wa Kiswahili kwamba Maadhimisho ya Siku ya Kiswahili Duniani yataendelea kuwa jukwaa muhimu la kuwakutanisha wapenzi wa lugha ya Kiswahili ili kujadili maendeleo ya lugha yao na kuweka mikakati ya kuzikabili changamoto zinazojitokeza ili Kiswahili kipige hatua zaidi na kuwawezesha kimapato watumiaji wake na nchi kwa ujumla.

HABARI KITAIFA

# Kampuni mama ya Tembo Nickel yauza hisa Marekani

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI mama ya Tembo Nickel, Lifezone Metals, jana imeanza kuuza hisa zake kwenye Soko la Hisa la New York (NYSE).

Taarifa iliyotolea na Kampuni ya Tembo Nickel kwa vyombo vya habari ilisema, Lifezone Metals ilitangaza nia yake ya kuweka hisa zake NYSE Desemba 2022 na sasa imefikia hatua hii kubwa.

Taarifa hiyo ilisema uhusiano wa Tanzania na Marekani ni muhimu kutokana na Rais Samia Suluhu Hassan kumkaribisha Makamu wa Rais wa Marekani, Kamala Harris, jijini Dar es Salaam, mwezi Machi, mwaka huu, kuonesha ukuaji wa uhusiano wa kimkakati kati ya nchi hizo mbili na mchango mkubwa wa Tanzania kama nchi inayochipukia katika uzalishaji wa madini ya kimkakati.

Mradi wa Kabanga Nickel ni moja kati ya mikubwa duniani ya madini ya nikeli ya kiwango cha juu ambacho hakija endelezwa. Kwa kutumia Teknolojia ya Hydromet waanzilishi wa kampuni ya Lifezone Metals wameongoza njia, Kabanga itaendelezwa kwa namna ambayo itapunguza uzalishaji wa hewa ya ukaa na kwa gharama ndogo, kwa lengo la kutengeneza metali za betri zinazohitajika duniani, hadi sasa.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Tembo Nickel, Benedict Busunzu, alisema hayo katika sherehe ya kupiga kengele ishara ya kampuni ya Lifezone Metals kuingia katika Soko la Hisa la New York Stock Exchange:

"Tuna furaha kubwa kueleza kwamba Tembo Nickel, kampuni yetu inayotekeleza Mradi wa Kabanga, inapiga hatua kubwa kila siku na hii inauthibitishia ulimwengu ni kwa namna gani mradi huu unaweza kubadilisha hali iliyopo sasa ya mchakato wa uchimbaji metali. Tunajivunia Kabanga na Tanzania kuwa mfano wa kuigwa kwa hili.

Tunaamini kwamba hatua ya Lifezone Metals kuwa kampuni ya umma imetuongezea ithibati moja zaidi. Ni heshima kuwa katika mwanzo huu rasmi leo wa kuuza hisa na hii ina maana kubwa sana kwangu na kwa Watanzania wenzangu.

Tunaipeleka Tanzania katika soko la Marekani kupitia hadhi ya Lifezone Metals kuwa kampuni ya umma." Taarifa hiyo ilisema Kampuni ya Kabanga Nickel itazalisha ajira, ujuzi na kuleta viwango vya juu vya usaidizi wa jamii husika zinazozunguka eneo la mradi katika Wilaya ya Ngara na maeneo mengine.

Uzalishaji wa kazi mpya hadi kufikia 900 unatarajiwa katika kambi tukikaribia kilele cha ujenzi.

Vilevile zaidi ya kazi mpya 270 zinatarajiwa katika Kiwanda cha Kuchakata Metali cha Kahama.

Tembo Nickel inaendelea kufanya kazi kwa ubia na Serikali ya Tanzania kwa mgawanyo sawa wa manufaa kutoka katika Mradi wa Kabanga Nickel.

Lifezone Metals ni kampuni ya kisasa. Kampuni mama ya Tembo Nickel na ina utaalamu katika metali utakaoiwezesha Tembo Nickel kuendeleza Mradi wa Kabanga.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Angellah Kairuki (kulia), akipokea kitabu cha taarifa mbalimbali ikiwamo ya miradi ya maendeleo ya Mkoa wa Tanga kutoka kwa Mkuu wa Mkoa huo, Waziri Kindamba, kabla ya kuanza ziara yake ya siku moja wilayani Korogwe jana. Katikati ni Mkuu wa Wilaya ya Korogwe, Jokate Mwegelo. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

# Simbachawene awacharukia watumishi wapenda rushwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, amekemea vitendo vya rushwa na ubinafsi vinavyofanywa na baadhi ya maofisa utumishi wa halmashauri nchini kwa watumishi wenzao wa ngazi za chini.

Alisema tatizo kubwa walilonalo baadhi ya maofisa utumishi ni rushwa, ukiritimba na ubinafsi uliowajaa badala ya kufanya kazi kwa kufuata maadili ya kazi ikiwamo kuwahudumia watumishi wanaowategemea kwa ajili ya kutatuliwa kero zao.

Simbachawene alisema hayo jana, wakati akifunga mafunzo kwa maofisa hao wa halmashauri zote nchini, pamoja na watumishi kutoka Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania (TSC), katika mkutano uliofanyika jana jijini Dodoma.

"Wamekuwa wakidai rushwa kuanzia Shilingi milioni tano hadi 10, jambo ambalo halikubaliki na atakayebainika atachukuliwa hatua kali," alionya.

"Maofisa Utumishi ndiyo chanzo kikubwa cha malalamiko kwa watumishi, acheni hiyo dhambi badala yake wahudumieni walimu na watumishi wengi kwa maadili," alisisitiza.

Akifafanua kuhusu suala hilo, Simbachawene alisema wamekuwa wakifanya kazi kwa hasira dhidi ya watumishi wanaokuja kutaka msaada kwao, ikiwamo wanaofuatilia utatuzi wa kero mbalimbali zinazowakabili katika maeneo wanayofanya kazi na kutaka baada ya kikao hiko cha pamoja wanapaswa kubadilika kiutendaji.

Alimwagiza Katibu Mkuu wa wizara hiyo kuhakikisha fedha inatafutwa ili kuunda vikosi kazi vitatu kila wilaya ambavyo vitapaswa kuwafuata walimu katika maeneo yao ya kazi kusikiliza changamoto zao na kuziingiza katika mfumo wa kiutumishi kwa ajili ya kufanyiwa kazi na mamlaka husika.

Kadhalika, Simbachawene alitoa miezi minne kuanzia sasa suala hilo linafanyika huku akitoa mwezi mmoja kwa Katibu Mkuu huyo fedha zinapatikana kwa ajili ya kuanza mchakato wa kuwatembelea watumishi hususani walimu katika maeneo ambayo wanafanyia kazi na kusikiliza changamoto zao.

Alisema anatarajia kuanza ziara Julai 14 katika wilaya mbalimbali nchini, lengo ikiwa ni kubaini kero zilizotolewa na zinazoendelea kutolewa na kusisitza kuwa, Ofisa Utumishi yeyote atakayebainika na tuhuma hizo, hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

"Naamini siyo maofisa utumishi wote wanaofanya vitendo vya rushwa, lakini asilimia kubwa ugonjwa huo wanao."

Alisema Agosti mwakani kwa mujibu wa maelekezo ya Rais, kusiwe na malalamiko yoyote kutoka kwa walimu.

Ili kuthibitisha suala hilo linafanyiwa kazi, alisema yeye kwa kushirikiana na Waziri wa TAMISEMI watawasilisha kwa Rais ombi la magari 139 pamoja na kompyuta mpakato kwa ajili ya maofisa utumishi ili iwe rahisi katika utendaji kazi wao.

Aliagiza walimu wapandishwe vyeo, madaraja huku akitoa miezi minne kwa maofisa utumishi kufuatilia suala hilo na kuliwasilisha katika mamlaka husika ili lifanyiwe kazi.

Aliwataka watumishi wote wavae beji ili waweze kubainika kwa mazuri au mabaya wanayofanya dhidi ya watumishi wao na wananchi kwa ujumla na kuongeza kuwa lazima kila taasisi iwe na mkataba wa huduma kwa wateja.

Hata hivyo Simbachawene ameishukuru serikali kwa kutoa vibali vya ajira kwa watumishi wa kada mbalimbali pamoja na kulipa baadhi ya malimbikizo ya madeni ya watumishi.

Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania (TSC), Paulina Mkwama, aliishukuru serikali kwa kuwaongezea bajeti, ikiwamo kuwapatia vitendea kazi na wanatarajia kupokea magari 16 pamoja na kompyuta 159 kwa ajili ya shughuli mbalimbali za tume hiyo.

# Serikali yawaondoa hofu wanaoishi na VVU

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

SERIKALI imewatoa wasiwasi watu wanaoishi na virusi vya Ukimwi (WAVIU) kuwa wataendelea kupata huduma zote baada ya bajeti ya mapambano dhidi ya virusi vya Ukimwi kuongezeka kutoka Sh. bilioni 14 hadi bilioni 25 mwaka 2023/24.

Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, Ummy Nderiananga, alisema hayo wakati alipowatembelea watu wanaoishi na virusi vya Ukimwi katika Halmashauri ya Mji Njombe.

"Rais mwaka jana kupitia TACAIDS alitutengea Sh. bilioni 14, lakini mwaka huu akasema inabidi niongeze tena kwenye eneo hili kwa hiyo mwaka ambao tumemaliza Bunge la bajeti tutakuwa na bilioni 25 na ushee kwa hiyo msiwe na wasiwasi dawa zitapatikana, huduma zote ambazo mnaendelea kuzipata mtaendelea kuzipata kama kawaida," alisema Ummy.

Alitoa rai kwa wananchi kuendelea kupima na kutambua hali zao na pindi wakikutwa na maambukizi watumie dawa za kufubaza na kuepuka unyanyapaa.

Pia, aliwaagiza wakurugenzi nchini mikopo ya asilimia 10 itakaporejeshwa kipaumbele kitolewe kwa vikundi vya watu wanaoishi na virusi vya Ukimwi.

"Sisi tunawategemea kwenye kuinua uchumi wa mtu mmoja mmoja, wa familia na taifa kwa ujumla kwa hiyo muwape kipaumbele na Mungu akijalia tutarudi tena kuja kuangalia," alisema Ummy.

Mratibu msaidizi wa mradi wa Hebu Tuyajenge, Agnes Nyoni, akizungumza kwa niaba ya Ofisa Mtendaji wa Baraza la Taifa la watu wanaoishi na virusi vya Ukimwi (NACOPHA), aliishukuru serikali kwa kuendelea kutoa mikopo kwa vijana wanaoishi na virusi hivyo pamoja na vijana balehe.

Mratibu wa Ukimwi Halmashauri ya Mji Njombe, Daniel Mwasongwe, alisema imefanikiwa kuwafikia wateja wapya 12,717 katika huduma ya upimaji kwa kipindi cha mwezi Januari hadi Machi, mwaka huu na kuunganishwa na huduma ya dawa kwa waliokutwa na VVU.

Katibu wa kikundi cha JIUKU, Rajabu Mligo, alimweleza Naibu Waziri kuwa wanaendelea na shughuli mbalimbali za ujasiriamali ikiwamo kilimo cha parachichi, mboga na ufugaji jambo ambalo linawasaidia kupunguza makali ya maisha.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ni umuhimu somo dawa za kulevya kufundishwa shuleni

**TATIZO** la matumizi ya dawa za kulevya duniani, limekuwa ni janga kwa vijana wengi na hata watu wazima.

Janga hilo pia limeikumba Tanzania kutokana na vijana wengi kujiingiza katika matumizi ya dawa hizo na kusababisha nguvu kazi kubwa ambayo taifa imekuwa ikiitegemea kupotea.

Biashara ya dawa za kulevya imeenea duniani kutokana na wanaofanya biashara hiyo kutajirika haraka na kuwa na matumizi ya anasa yanayowavutia vijana kuyaiga na kuishia kupotea.

Wazazi wengi wamepoteza watoto wao ambao wamewahangaikia kuwalea na kuwasomesha kwa gharama kubwa, lakini kuishia kwenye biashara au matumizi ya dawa hizo.

Wengi huishia kufungwa vifungo vya maisha na wengine hupoteza maisha kwa sababu ya kuzidisha matumizi ya dawa hizo.

Taarifa kwamba kuna mchakato wa kuliweka somo la dawa za kulevya kwenye mitaala kuanzia elimu ya msingi, zinaleta matumaini ya kuwaokoa vijana wengi kujiingiza katika matumizi ya dawa hizo.

Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), Aretas Lyimo, amebainisha kuwa kuna mchakato unaendelea kuingiza somo la elimu ya dawa za kulevya kwenye mitaala ili somo hilo lifundishwe kuanzia shule ya msingi mpaka vyuo kuepusha kundi kubwa la Watanzania kuingia kwenye dawa za kulevya.

"Tumeandaa mwongozo wa ufundishaji ambao kupitia Wizara ya Elimu na wadau wetu mbalimbali wanafunzi watafundishwa juu ya uelewa wa dawa za kulevya jinsi ya kuepukana nazo na madhara yake kwa ujumla, hii yote ni kuhakikisha tunakomesha tatizo hili," anasema.

Pia kuna jitihada zinazofanywa kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo kufanya utafiti na operesheni nchi nzima ili kubaini mikoa iliyokithiri kwa kujihusisha na kilimo cha dawa za kulevya ikiwamo bangi na mirungi na kuwawezesha wahusika kufanya shughuli zingine ili kuachana na kilimo hicho.

Mikoa inayotajwa kuongoza kwa kilimo cha bangi ni Arusha, Mara, Morogoro, Ruvuma na Iringa na inayolima mirungi ni Tanga na Kilimanjaro ambako kote elimu itatolewa na kufanyika utafiti wa kuja na mazao mbadala.

Vile vile, imebainika kuwa jamii ya Watanzania bado haijachukua jukumu la kupambana na dawa za kulevya ikiwamo kuelimisha watu kuhusu athari na ubaya wa dawa hizo na kwamba wazazi wengi hawachukui jukumu hilo na kulinda watoto wao.

Viongozi wa kimila, kidini, vijiji na vitongoji hadi wa ngazi za juu na jamii kwa ujumla, kwamba kila mmoja kwa nafasi yake angekuwa anakemea jambo hilo na kuhakikisha sehemu yoyote linapotokea wanachukua hatua kukemea suala la athari za dawa hizo kwa jamii lisingekuwa kubwa kiasi hicho.


Vijana wengi wanaangamia, ukipita kwenye vituo vya basi utagundua jinsi dawa hizo zilivyobadilisha maisha yao na kuwa kama mazezeta.

Wengine utawakuta wamesinzia huku wamesimama na midomo yao imebadilika rangi nakuwa mweusi na mate yakiwatoka bila kujitambua.

Dawa za kulevya wanazotumia, zinawafanya pia wajiingize kwenye ukwapuaji wa abiria wanaopanda mabasi ili waweze kupata pesa ya kununulia dawa hizo.

Hatua zisipochukuliwa vijana wengi wataendelea kuangamia na taifa kukosa nguvu kazi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# Siioni dhamira ya kuwaondoa machinga maeneo yasiyo rasmi

**MAAGIZO** kwa halmashauri kuwatengea machinga maeneo ya kufanyia biashara zao yalishatolewa na viongozi wakuu wa serikali mara nyingi. Lakini hadi sasa wafanyabiashara hao wanaendesha shughuli zao katika maeneo yasiyo rasmi.

Lengo la kuziagiza halmashauri kutenga maeneo kwa ajili ya kundi hilo ni kutaka wafanyabiashara wadogo hao kuendesha shughuli zao bila kuvunja sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa na serikali.

Ili kufanikisha utengaji wa maeneo hayo, wakuu wa wilaya walishaelekezwa kuratibu na kuhakikisha maeneo ya kufanyia biashara yanatengwa na halmashauri.

Sasa iko wazi - machinga kutengewa maeneo ya kufanyia biashara inawezakana, lakini kuwaondoa katika maeneo yasiyo rasmi ni mfupa ulioshindikana. Wako mitaani wanaendelea na biashara kama kawaida.

Serikali inakiri machinga ni watu muhimu katika kukuza uchumi wa Tanzania kwa kuwa wafanyabiashara wadogo ndio wanaoleta muunganiko wa watu katika kada mbalimbali.

Wanaotajwa na serikali katika mnyororo huo ni wasomi wenye shahada, astashaada, kidato cha sita, kidato cha nne, darasa la saba na wasiosoma kabisa, wote huunganika na kufanya biashara kama machinga.

Kuna kipindi aliyekuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) mwaka 2018, Dk. Seleman Jafo, kuwa kati ya Watanzania milioni 50, walioajiriwa serikalini na sekta ya umma ni 520,000 kwa wakati huo.

Dk. Jafo ambaye kwa sasa ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais -Muungano na Mazingira, alisema kundi kubwa ni la watu ama wamejiajiri au wameajiriwa katika sekta binafsi.

Kwa kuzingatia maelezo hayo, ni wazi kwamba kundi la machinga linatakiwa kushikiliwa ili lichangie katika uchumi wa nchi badala ya kuliacha likitangatanga kama ilivyo sasa.

Yawezekana kukawa na changamoto kutoka kwa machinga wenyewe au halmashauri, kwani kumekuwapo malalamiko kutoka kwa kundi hilo kwamba maeneo au masoko wanayopelekwa, hayana miundombinu rafiki kwa biashara zao. Hayatoshi, hayafikiki kirahisi, hayana huduma muhimu kama maji na vyoo.

Kutokana na malalamiko hayo, Rais wa awamu ya tano, Dk. John Magufuli (hayati) mwaka 2016 alisitisha mtindo wa kuwahamishia machinga katika masoko hayo hadi miundombinu iboreshwe.

Swali ni je, tangu wakati huo hadi leo miundombinu haijaboreshwa? Kwanini wanaendelea kufanya biashara katika maeneo yasiyo rasmi na kuhatarisha maisha yao na ya wengine?

Juma hili, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, ametoa maagizo kama hayo, huku akikisitiza halmashauri zote nchini, ukiwamo uongozi wa Mkoa wa Dar es Salaam, kuweka utaratibu wa kuwapanga machinga katika maeneo rafiki, ili wafanye biashara zao kwa uhuru na kuchangia uchumi wa taifa.

Ni katika hafla ya uzinduzi wa Maonyesho ya 47 ya Biashara ya Kimataifa, maarufu Sabasaba, anasisitiza maeneo ya machinga yawekwe miundombinu muhimu, akilitolea mfano Soko la Machinga jijini Dodoma.

Kwa mujibu wa Waziri Mkuu, lengo la serikali ni kutengeneza mabilionea kupitia biashara. Ni fahari kwa nchi kuona machinga wanakuwa na kufanya biashara kimataifa.

Waziri Mkuu anataka Mkoa wa Dar es Salaam kuwa na eneo la kufanya biashara saa 24. Kwa kauli hiyo, ni wazi serikali imedhamiria kuwainua machinga, hivyo ni vyema halmashauri zikatekeleza.

# Polisi kuajiri askari wapya 3,000

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI inakusudia kujenga vituo bora vya polisi katika kata zote nchini ambavyo vitafanya kazi saa 24 huku Jeshi la Polisi likitarajia kuongeza askari wapya 3,000.

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, alibainisha hayo jana alipokagua hali ya ulinzi na usalama katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Julius Nyerere (JNIA) jijini Dar es Salaam.

Masauni alieleza kuridhishwa na hali ya ulinzi na usalama katika uwanja huo na kueleza nia ya serikali kuimarisha Jeshi la Polisi, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji na Jeshi la Uhamiaji.

Waziri huyo alisema nia ya serikali ni kujenga vituo vya polisi katika kata zote nchini ili kutoa huduma kwa wananchi kwa ufanisi.

“Kikubwa ambacho nimejifunza katika ziara hii ni uwekezaji mkubwa uliofanywa na serikali katika kuimarisha usalama katika uwanja huu. Mazingira haya yanaendana pia kuwalinda wawekezaji wetu wakubwa wanaokuja kuwekeza nchini,” alisema Masauni.

Alikosoa alichokiita propaganda zinazofanywa na baadhi ya watu kuhusu wawekezaji na kueleza usalama uliopo uwanjani huko ni kielelezo tosha cha namna serikali ilivyojipanga kutoa huduma kwa wawekezaji.

Kamishna wa Jeshi la Polisi Utawala na Rasilimali Watu, Suzane Kaganda, alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa maboresho makubwa ambayo serikali inafanya katika utendaji wa jeshi hilo.

Alisema Rais Samia ameelekeza zitolewe ajira 3,000 za polisi wapya ambao watasambazwa nchi nzima, jambo alilolitaja litaongeza ufanisi kiutendaji.

“Tunamshukuru Rais kwa kutoa ajira hizo 3,000, malengo yetu ni kuwa na idadi kubwa ya askari lakini katika dhana hiyo hiyo ya kuwashirikisha wananchi,” alisema Kamishna Kaganda.

Alisema katika dhana hiyo, Jeshi la Polisi litapeleka askari kata wanaoshirikiana na vikundi vya ulinzi shirikishi ikiwa ni jitihada za kuhakikisha Watanzania wanakuwa salama.

Alisema kwa sasa vituo vidogo vya polisi havifanyi kazi saa 24. Vituo hivyo vya kata vitakapokamilika vitafanya kazi saa 24, hivyo kutoa huduma kwa wananchi kwa wingi.




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akifurahia jambo na wafanyakazi wa Tigo Tanzania, katika banda la TEHAMA, kwenye maonyesho ya 47 ya biashara ya kimataifa Dar es Salaam, viwanja vya Sabasaba barabara ya Kilwa juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kizimbani mashtaka kubaka na kumwambukiza VVU dada yake

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

DEOGRATIAS Wiliamu (43), mkazi wa Mtaa wa Mombasa Raha, Kata ya Butundwe, amesomewa maelezo ya awali katika mashtaka yanayomkabili ya kubaka na kumwambukiza Virusi vya Ukimwi (VVU) kwa makusudi mdogo wake, msichana mwenye umri wa miaka 17.

Mshtakiwa huyo alisomewa maelezo hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Geita, Nyakato Bigirwa.

Hata hivyo, mshtakiwa huyo alikana na kuhusika na makosa yote mawili. Yuko mahabusu katika Gereza la Wilaya ya Geita kutokana na kukosa wadhamini.

Upande wa Mashtaka, ukiongozwa na Mawakili wa Serikali, Godfrey Odupoy na Kabula Benjamini, ulidai mahakamani huko kuwa upelelezi wa kesi hiyo umekamilika na kuomba mahakama hiyo umsomee mshtakiwa huyo maelezo ya awali.

Hakimu Bigirwa alikubaliana na ombi hilo na kumwuliza mshtakiwa kama alikuwa tayari kusomewa maelezo ya awali. Alikubali.

Akisoma maelezo ya awali, Wakili wa Serikali Odupoy alidai kuwa katika tarehe tofauti kati ya mwaka 2018 na 2023, katika mtaa wa Mombasa Raha, Kata ya Butundwe, Mkoa wa Geita, msichana huyo alikuwa anaishi na kaka yake ambaye ni mshtakiwa Deogratias Wiliamu, alikuwa anambaka huku akimtishia kwa kudai kuwa iwapo angemwambia mtu yeyote, angempiga fimbo na kumchoma kisu.

Wakili Odupoy alidai binti huyo alipougua, mshtakiwa huyo alimpeleka kituo cha afya na alipofanyiwa vipimo, alibainika kuwa na VVU na baada ya majibu hayo kutolewa, siku iliyofuata mshtakiwa alimpiga mdogo wake huyo ambaye jina lake tunalo.

Alidai kuwa baada ya kumpiga, mdogo wake huyo alikimbia na kwenda kwa mama yake Raheli Masanyiwa na kumweleza kuwa “kaka yangu Deogratias Wiliamu alikuwa akinibaka kila siku na kuniambukiza VVU na sasa ninatumia vidonge vya kupunguza makali ya VVU”.

Wakili huyo aliendelea kudai kuwa baada ya mama huyo kupewa taarifa hizo, aliwaita ndugu zake na mshtakiwa, lakini mshtakiwa huyo hakufika kwenye kikao hicho cha familia. Kikao kilifanyika na msichana huyo alieleza kila kitu alichokuwa anafanyiwa na kaka yake.

Alidai kuwa kikao hicho cha familia kiliamua kulifikisha suala hilo Kituo cha Polisi Katoro kutoa taarifa na msichana huyo alipewa Fomu Na. 3 ya Polisi (PF3) na kwenda katika Kituo cha Afya Katoro na alipofanyiwa vipimo, alibainika kubakwa, pia ana VVU.

Wakili huyo alidai kuwa baada ya kugundulika kuwa alibakwa na pia ana VVU, polisi walimsaka mtuhumiwa na kumkamata. Upelelezi ulipokamilika walimpeleka mahakamani ili sheria ichukue mkondo wake.

Alidai kuwa Upande wa Mashtaka unatarajia kupeleka mahakamani huko mashahidi watano na vielelezo viwili na kuomba mahakama hiyo ipange tarehe nyingine kwa ajili ya kuanza kusikiliza kesi hiyo.

Hakimu Bigirwa alikubaliana na ombi hilo na kuahirisha kesi hiyo hadi Julai 19 mwaka huu kwa ajili ya kuanza kusikilizwa.

Hakimu Bigirwa aliyataja masharti ya dhamana kwa mshtakiwa huyo kuwa anatakiwa awe na wadhamini wawili wenye barua ya utambulisho kutoka kwa Ofisa Mtendaji wa Kata na mali isiyohamishika yenye thamani ya Sh. milioni tano.

Akisoma hati ya mashtaka, Wakili wa Serikali Odupoy alidai kuwa katika tarehe tofauti, kati ya mwaka 2018 na 2023, katika Mtaa wa Mombasa Raha, Kata ya Butundwe, mkoani Geita, mshtakiwa alimbaka mdogo wake huyo, msichana mwenye umri wa miaka 17 na kumwambukiza VVU kwa makusudi. Ni makosa yanayokiuka sheria za nchi, ikiwamo inayohusiana na VVU/Ukimwi ya mwaka 2008.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# NSSF yataja sababu ucheleweshaji mafao

**Na Beatrice Shayo**

UONGOZI wa Mfuko wa Hifadhi wa Jamii (NSSF) umesema ucheleweshaji wa mafao kwa mwanachama unasababishwa na mhusika kutokukamilisha taarifa zake kwa wakati na waajiri kutokupeleka michango yao.

Kaimu Mkurugenzi wa NSSF, Robert Kadege, alibainisha hayo jana katika banda lao kwenye Maonesho ya 47 ya Biashara ya Kimataifa (Sabasaba) yanayoendelea Viwanja vya Mwalimu Nyerere mkoani Dar es Salaam.

Alisema moja ya kazi kubwa wanayoifanya ni kushughulikia kero za wanachama na malalamiko ya ucheleweshaji wa mafao yanayosababishwa na kukosekana kwa taarifa zilizokamilika.

"Kwa dai ambalo taarifa zake zipo sahihi, ndani ya siku 30 tunao uwezo wa kulilipa, lakini ikitokea tunatakiwa kulimpa mwanachama sasa hivi ni lazima taarifa za mwanachama zioane na taarifa zake zilizoko katika Mamlaka ya Vitambulisho ya Taifa (NIDA).

"Taarifa za NIDA zinatakiwa kulingana na taarifa alizotuletea ila kwa yule ambaye taarifa zake zipo sahihi analipwa kwa wakati. Hakuna ucheleweshaji taarifa za mwanachama zinapokuwa zipo sahihi," alisema Kadege.

Kaimu Mkurugenzi huyo alitaja jambo lingine linalosababisha madai kuchelewa ni baadhi ya waajiri kutokuwasilisha michango ya wanachama kwa wakati.

Kadege alisema waajiri ambao hawawasilishi michango ya watumishi wao, huchukuliwa hatua mbalimbali, japo hawajafikia hatua ya mwisho ya kuwafikisha mahakamani.

"Hatua ya mahakamani ni jambo la mwisho lakini kwa kawaida huwa tunashirikisha vyombo mbalimbali kwa lengo la kusaidiana ili kupata hiyo michango," alisema.

Alibainisha kuwa ikishathibitika mwanachama alikatwa makato katika mshahara wake, mfuko una wajibu kufuatilia ili apatiwe haki yake.

"Ndio maana mmesikia kama miezi miwili iliyopita tulienda kukamata mali za kampuni moja ili zipigwe mnada na kufidia madeni ya mchango, yote hayo ni kuhakikisha michango ya wafanyakazi inawasilishwa katika mfuko ili tuwalipe wanachama wetu stahiki zao," alisema.

Alisema wameboresha mifumo yao ya Tehama katika kushughulikia mafao na kwa sasa hivi taarifa zote wakishazipata dai hilo linashughulikiwa kielektroniki na mwanachama atayakuta mafao yake benki.

Alibainisha kuwa thamani ya mfuko imeendelea kukua kutoka Sh. trilioni 4.7 Machi 2021 hadi Sh. trilioni 6.87 Machi 2023, ongezeko likichagizwa na idadi ya wanachama kuongezeka.




Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA), Hamza Johari, akizungumza na wafanyakazi wa mamlaka hiyo kwenye maonyesho ya 47 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam alipotembelea banda hilo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# UDOM yaibuka na 'greenhouse' mpya

**Na Christina Mwakangale**

CHUO Kikuu cha Dodoma (UDOM) kimebuni mfumo madhubuti unaodhibiti hali ya hewa, ikiwamo unyevunyevu na joto katika kilimo cha kitanda nyumba (greenhouse).

Lengo la kuweka urahisi kwa mkulima kubaini aina za mazao yanayostahili kulimwa kulingana na mazingira ya eneo husika.

Paschal Magambo, mwanataaluma kutoka Idara ya Fizikia, Ndaki ya Sayansi Asilia na Hisabati UDOM, alieleza utendaji wa ubinifu wao alipozungumza na mwandishi kwenye banda la chuo hicho katika maonesho ya Sabasaba.

Alisema teknolojia iliyobuniwa na chuo hicho ni tofauti na teknolojia zingine za kilimo hicho zilizoko sokoni, utafiti wao kabla ya ubunifu huo ulibaini zilizopo nchini hazina uwezo wa kudhibiti hali ya hewa kulingana na eneo husika.

"Tofauti kati ya 'greenhouse' zilizopo, zimejengewa tu, lakini ndani hazidhibiti hali ya hewa iliyopo ndani. Kwa mfano 'greenhouse' ya hapa Dar es Salaam na iliyopo Mafinga au Makete kwenye baridi, zikifanana, si sawa.

"Kufanana kwa 'greenhouse' wakati mazingira ni tofauti ya joto na baridi kunamfanya mkulima asibaini ni zao gani linafaa eneo hilo. Nikaona nije na hii 'greenhouse control system', unaweza kuchagua aina ya zao, mfano tikiti au nyanya na itakuonyesha ni joto la aina gani linahitajika, ili zao likue," alisema Magambo.

Alisema ubunifu huo umefanyiwa majaribio na kubaini unaweza kujibadilisha kulingana na mazingira ya sehemu mbalimbali, kwa kutumia kifaa maalum kitakachofungwa kwenye 'greenhouse', tofauti na zilizoko sokoni hivi sasa, zimetengenezwa kudhibiti wadudu pekee.

Magambo alisema ubunifu huo ni rahisi kutumiwa na mkulima mwenye elimu ya kiwango chochote, kwa kuwa mfumo unajidhibiti na kwamba kifaa kinachotumika kupima hali hewa hutumia nishati ya umeme au ya jua.

Mkufunzi wa chuo hicho, Dk. Ombeni Mdee, alisema UDOM imeendelea na ubunifu katika maeneo tofauti huku ikibuni pampu ya maji inayotumia umeme mdogo, ili kupunguza matumizi ya nishati hiyo.

# TFS yapata mbinu udhibiti wa moto

**Na Elizabeth Zaya**

WAKALA wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) umesema mfumo wa kudhibiti matukio ya moto kwa njia ya kidijitali umesaidia kupunguza uharibifu wa mapori na misitu ambao ulikuwa unatokana na kukithiri kwa matukio hayo miaka ya nyuma.

Mtaalamu wa kufuatilia moto wa msituni kwa njia ya satelaiti kutoka TFS, Kekilia Kabalimu, alibainisha hayo alipozungumza na Nipashe katika banda lao kwenye maonesho ya Sabasaba mkoani Dar es Salaam.

Alisema tangu waanze kutumia mfumo huo wa udhibiti, matukio ya moto yamepungua kwa kiwango kikubwa.

"Kwa kutumia mfumo huu popote moto unapowaka ni lazima tuuone na tuchukue hatua za haraka kudhibiti na kupitia mifumo hii ya kidijitali, inatusaidia kutupa taarifa bila kujali umbali wa eneo moto unapowaka," alisema Kekilia.

"Na kupitia mfumo huu, huwa unaonyesha eneo moto ulipo, tarehe na muda ulipoanza kuwaka, hii kwetu huturahisishia namna ya kufuatilia na kudhibiti kabla haujaleta madhara zaidi," alisema.

Alibainisha kuwa tayari wameshaanza kutoa elimu kwa jamii zinazozunguka misitu na mbuga zote kuhusu mfumo huo ili na wao wautambue.

Alisema mfumo huo ulianza kutumiwa mwaka 2011 na umewasaidia kupunguza matukio ya moto katika maeneo yaliyokuwa yanachomwa moto mara kwa mara.

"Na wananchi wamekuwa na uelewa na tumeona tuwe na mafunzo endelevu kuhusu eneo hili kwa sababu tunaona lina umuhimu mkubwa na tunaamini huu ndio mwarobaini kwa majanga ya moto ambayo yanaharibu misitu yetu," alisema Kekilia.

# GEL yafanya udahili Sabasaba wanaotaka kusoma nje ya nchi

**Na Joseph Mwendapole**

WAKALA wa Elimu Nje ya nchi, Global Education Link (GEL) unadahili wanafunzi wanaokwenda kusoma vyuo vikuu nje ya nchi katika maonyesho ya Sabasaba yanayoendelea mkoani Dar es Salaam.

Meneja Mkuu wa GEL, Regina Lema, alisema jana kuwa wameamua kwenda Sabasaba ili kufanya urahisi wa udahili kwa wanafunzi waliohitimu kidato cha sita wanaotaka kwenda kusoma vyuo vikuu nje ya nchi.

Alisema pia wanadahili wanafunzi waliohitimu stashahada ambao wanataka kwenda kusoma katika vyuo vikuu vinavyopatikana nje ya nchi.

"Kwa sasa tunadahili wanafunzi wanaotaka kwenda kuanza vyuo vikuu nje ya nchi kuanzia Septemba mwaka huu na hapa tunasajili mwanafunzi ndani ya saa 24.

"Wanaofika hapa tunawapa ushauri wa bure kuhusu kozi wanazotaka kusomea na vyuo ambavyo vitawafaa na kozi zao na tunawaonyesha fursa zilizopo za ufadhili katika vyuo mbalimbali," alisema.

Regina aliwataka wahitimu wa kidato cha sita kuchangamkia fursa ya kwenda katika maonesho ya Sabasaba na kutembelea banda la Global Education Link ili kuangalia fursa mbalimbali zinazopatikana.

Kuhusu mikopo kwa wanafunzi wanaokwenda kusoma nje ya nchi, Regina alisema Global Education Link wanakopesha mzazi ambaye anapaswa kurejesha ndani ya miezi minane baada ya mtoto wake kupata udahili na kwenda nje ya nchi.

Alisema mikopo hiyo haina riba. Mzazi anaweza kukopeshwa hadi Sh. milioni 10 na akikamilisha taratibu za kupata mkopo huo, ataupata ndani ya saa 24.

Regina alisema kila mwaka wanadahili zaidi ya wanafunzi 700 wanaokwenda kusoma nje ya nchi na wamekuwa wanafuatilia maendeleo yao hadi wanapohitimu.





## AMCOS, APK waingia makubaliano kuzalisha sharubati

**Na Mary Mosha,** HAI

CHAMA cha Ushirika wa Kilimo na Masoko (AMCOS) cha Lyamungo kwa ushirikiano na kampuni ya uwekezaji ya kahawa ya African Plantations Kilimanjaro Limited (APK), wameingia ushirikiano wa kuzalisha sharubati kwa kutumia coffee pulps.

Hayo yalisemwa jana na Mwenyekiti wa AMCOS wa Lyamungo, aliyemaliza muda wake, Gabriel Ollomi, wakati wa mkutano mkuu wa chama hicho sambamba na kuingia madarakani kwa uongozi mpya wa chama hicho.

"Hii itakuwa ni mara ya kwanza kwa aina hii kuzalishwa hapa nchini na mazungumzo yetu ya awali kati ya uongozi wa Lyamungo AMCOS na APK Ltd yataleta manufaa kwa kuwa makubaliano yetu ni kuwa chama hiki cha ushirika kitapata asilimia 10 ya mapato yatakayotokana na mauzo ya sharubati hiyo," alisema.

Aidha Ollomi, alisema uongozi huo ulifikia hatua hiyo baada ya viongozi wa chama hicho kufanya ziara kwenye baadhi ya nchi za Amerika Kusini zinazozalisha kahawa na kukuta sharubati inayotengenezwa kutokana na coffee pulsp.

"Tulikuta kinywaji hiki ni muhimu na kinapendwa haswa kwenye nchi za Colombia na Brazil hivyo tukafanya mazungumzo na APK Ltd ambao wamekodisha shamba letu kwa ajili ya kilimo cha kahawa kwa ajili ya kuzalisha kinywaji hicho ambapo itakuwa ni mara ya kwanza kabisa hapa nchini," alisema.

Aidha alisema chama hicho kimetenga Sh.milioni 150 kwa ajili ya kukusanya kahawa kilogramu 30,000 kupitia chama hicho katika msimu wa 2023/2024.

Baadhi ya wanachama wa chama hicho akiwamo Erasto Mallya, alisema kufanyika kwa jambo hilo kutarudisha dhamani ya zao la kuhawa hasa katika mnyororo wa thamani.

Waliochagulia kushika nyadhifa ya uongozi ni Mwenyekiti, John Nkya, Makamu Mwenyekiti Orgenes Mlula, pamoja na wajumbe wa bodi wakiongozwa na Elihuruma Mushi, Asanterabi Lema, Janeth Ndanshau, Reginald Massawe, Timotheo Kwayu, John Elimuu, Renalda Lema na Gamalieli Shoo.

# RC apiga marufuku madereva bajaji, daladala kutembea na sime, mapanga

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, John Mongella, amepiga marufuku madereva wa daladala na bajaji kubeba silaha ikiwamo sime, mapanga akisema kwa chombo kitakachokutwa na silaha hizo kitafutiwa leseni ya usafirishaji.

Alitoa agizo hilo jana jijini Arusha wakati akizungumza nao kwa ajili ya kupata suluhu ya kumaliza migomo inayojitokeza akisema leo atakutana na madereva wa bajaji kupata suluhu ya changamoto zao.

"Sitaki kusikia silaha zinawekwa katika magari haya, kwani ni hatari kwa usalama wao na wengine hasa pale inapotokea tofauti kati yao, pia sitaki kusikia mtu wa daladala kampiga mtu wa bajaji na mtu wa bajaji kampiga mtu wa daladala nikisikia hatua kali zitachukuliwa," alisema.

Alisema kusikiliza watu ni kujifunza zaidi na wote wanatafuta maisha, kwani bajaji ni ajira na daladala ni ajira na wanaofanya uwekezaji nao wanataka tija kwenye maisha yao.

"Daladala wanahoja zao na bajaji wanahoja zao lazima niwasilikize wote ili nijue wapi pakuanzia, angalieni mgomo wa juzi watu wazima wanapanda kirikuu na wanafunzi wanatembea inasikitisha, ofisi yangu haina mipaka unajua mimi ni baba, siwezi kutembea na viboko kila mahali, lakini nawaambia suala la migomo halileti afya hapa Arusha," alisema.

Kadhalika, alisema usafiri wa daladala unatumiwa hata na watalii na siku hizi teknolojia zipo, migomo haina afya na ndio maana nataka kila mtu awe huru kusema kinachowasibu, ili zitatuliwe.

"Hapa hakuna jambo la kipuuzi lakini ukiyasikia unaelewa mnahoja gani na nafuu siyo kwa kila anachosema daladala kitakuwa sawa na siyo cha bajaji kitakuwa sawa, naelewa michango yenu katika sekta ya usafirishaji na kamati niliyounda zamani ya kusimamia usafiri itarudi tena," alisema.

Pia alisema wakati mgomo ukiendelea aliona baadhi wakicheza mpira wa miguu na kugundua kuwa madereva daladala wanavipaji vya michezo, hivyo ataanzisha mashindano ya michezo ili kuibua vipaji vyao zaidi.

Aidha, wamemwomba Mongella kumwita Mbunge wa Arusha Mjini, Mrisho Gambo, kwenye kikao chao, ili athibitishe kama kweli anamiliki bajaji 350 kati ya 2,000 zilizopo jijini Arusha.

Madereva hao walilalamika uwepo wa bajaji nyingi ambazo hazilipi kodi, lakini zinaingiza mapato mengi kuliko daladala zinazolipa ushuru na kodi.

Naye Katibu Mkuu wa madereva wa daladala, Ramadhani Kapelenja, alihoji kama kweli Gambo anamiliki bajaji 350, lazima wajue ili zifuate utaratibu na nyinginezo kuondolewa.

"Lazima hizo fununu ziondoke na tujue kama mbunge anamiliki bajaji 350 tujue, ili serikali iziondoe nyingine maana zimezidi kwani sisi tunalipa kodi na ushuru, lakini wao tukifuatilia ushuru na kodi hawalipi, sasa tunaomba aitwe atueleze ni kweli anamiliki bajaji hizo au ni maneno maneno tu," alisema.

Nao wamiliki wa daladala, Locken Massawe ambaye ni Katibu wa Wasafirishaji Kanda ya Kaskazini (AKIBOA) aliomba wamiliki wa daladala wapate leseni kwa wakati na kama leseni imeisha, waingie katika mtandao waombe.

Pia aliomba njia zilizozuiliwa awali kama za Njiro badala ya kupita eneo la Friends Corner wapite Barabara ya NMB hadi Soko Kuu.



Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga na Msimamizi wa uchaguzi mdogo wa udiwani Kata ya Potwe, Dk. Jumaa Mhina (wa pili kulia), akiwaapisha mawakala kutoka vyama sita vya siasa katika ofisi ya Ofisa Mtendaji wa kata hiyo, katika kijiji cha Ndondondo jana. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Benki ya NBC yapongezwa kuanzisha malipo kidijitali

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

TAASISI na kampuni ambao ni wateja wa Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) mkoani Arusha, wameipongeza benki hiyo kwa kuwapelekea huduma ya malipo ya kidijitali iitwayo NBC Connect inayosaidia kuokoa muda na kuongeza ufanisi.

NBC Connect, ni huduma ya kisasa ya kidijitali kwa kampuni na taasisi mbalimbali, ambayo huwezesha huduma salama za kibenki kufanyika sehemu na muda wowote kwa njia ya mtandao.

Joseph Buko kutoka Kampuni ya Rhotia Valley, alisema pamoja na kusaidia kuokoa muda, mfumo huo utaongeza ufanisi kwa kuwa unaruhusu kufanya miamala mingi kwa wakati mmoja na kwa ufanisi.

"Tunaishukuru Benki ya NBC kwa kutuletea huduma hii nzuri. Kulingana na mawasilisho yao kwetu, ni wazi kuwa itatusaidia sana kuokoa muda na muhimu zaidi, kuongeza ufanisi katika shughuli zetu za kila siku," alisema.

Aidha, Yusuph Zege kutoka Chuo Kikuu cha Arusha, alishukuru Benki ya NBC kwa kuja na huduma hiyo ya kibunifu na kuongeza kuwa inaonyesha namna ambavyo benki hiyo inawafikiria na kuwajali wateja wake ambao ni taasisi binafsi na za serikali.


Mkurugenzi wa wateja wakubwa NBC , James Metairon, alisema: "Tunafuraha kutambulisha NBC Connect kwa wakazi wa Arusha. Mfumo huu wa kibenki wa kidijitali ni uthibitisho wa dhamira ya kuwapatia wateja wetu huduma bora za kibenki ambazo ni rahisi, salama na kukidhi mahitaji yao.

...NBC Connect itawawezesha wateja wetu wenye kampuni na taasisi mbalimbali kufanya huduma za kibenki popote pale, wakati wowote, na kufurahia huduma hizo bila matatizo."

Alisema: "Pamoja na huduma rahisi na za kisasa, NBC Connect itatoa usaidizi binafsi kwa wateja kupitia kituo chake cha huduma kwa wateja, mameneja wetu wanapatikana ili kuwasaidia wateja kulingana na mahitaji yao na kutoa mwongozo wa jinsi ya kutumia huduma hilo kwa ufanisi."

Katibu Tawala Msaidizi Mkoa wa Arusha, David Lyamongi, aliishukuru Benki ya NBC kwa ubunifu wao mzuri na kuwahimiza wateja kutumia mfumo huo mpya wa kibenki ili kurahisisha shughuli zao za kibenki.

Uzinduzi wa NBC Connect Arusha unawakilisha mpango mkakati wa upanuzi wa Benki ya NBC ili kufikia taasisi mbalimbali na kuchangia ukuaji wa uchumi wa nchi.





# Vyandarua milioni 1 kutolewa Kagera kudhibiti malaria

**Na Restuta Damian,** KAGERA

WAKAZI wa Mkoa wa Kagera wanatarajia kupewa msaada wa vyandarua zaidi ya milioni moja ili kudhibiti ugonjwa wa malaria kwa asilimia 18.

Hatua hiyo inakuja baada ya mkoa huo kushika nafasi ya pili kati ya mikoa mitano yenye kiwango cha juu cha ugonjwa huo.

Hayo yalibainishwa juzi na mwakilishi wa Naibu Katibu Mkuu wa Afya na Lishe kutoka Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Sebisya Kabuje wakati wa kikao cha uhamasishaji na udhibiti wa ugonjwa wa malaria kwa viongozi ngazi ya mkoa na wilaya.

Kabuje alisema kuwa kufuatia utafiti uliofanyika mwaka 2022 juu ya ongezeko la ugonjwa wa malaria ilibainika kuwa mikoa iliyo na kiwango cha juu cha maambukizi ni Tabora yenye asilimia 23, Kagera (18%), Mara (15%) Shinyanga (16%) na Mtwara (20%).

Alieleza kuwa kupitia usimamizi wa serikali mwaka 2017 maambukizi ya ugonjwa huo kwa nchi nzima yalikuwa asilimia 14.8 lakini hadi kufikia mwaka 2023 yalipungua mpaka kufikia asilimia 8.1.

Alisema katika kuendelea kutekeleza afua za afya ni lazima kuwe na ugawaji wa vyandaraua ngazi ya kaya, shule, na jamii kwa ujumla kwani mazalia na vimelea vya mbu husababishwa na hali ya usafi wa mazingira.

"Njia hizo kwa pamoja zinaweza kufanikiwa malengo ya serikali katika kutokomeza malaria kwa kuhakikisha kila kata inapata vyandarua na kutumia kwa usahihi na kutoweka kwenye kuvulia samaki na kuanikia dagaa," alisema Kabuje.

Aidha alisema kwa asilimia 93 ya Watanzania wapo katika hatari ya kuugua ugonjwa wa malaria ikiwa ni miongoni mwa nchi 10 za Afrika.

Mkuu wa Wilaya ya Bukoba, Erasto Siima, alisema katika kutekeleza zoezi ugawaji vyandarua Mkoa wa Kagera utaanza kwa uandikisha wenye kutambua idadi halisi ya wana kaya.

Alisema makundi ya wajawazito na watoto chini ya miaka mitano ndiyo yanayoathiriwa zaidi kwa taarifa zinazotoka kwenye hospitali na vituo vya afya, hivyo kupewa kipaumbele wakati wa utolewaji wa vyandarua hivyo.

Hata hivyo alisema shughuli ya ugawaji vyandarua itasimamiwa na viongozi wa mkoa na wilaya ifikapo Agosti mwaka huu kwa kuzingatia taratibu na malengo yanayokusudiwa na wadhamini na serikali.



Ofisa Uhusiano wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Kahama (KUWASA), John Mkama (aliyechuchumaa), akiwaonyesha wananchi wa Mtaa wa Mwime, Manispaa ya Kahama, namna Hamisi Omary mkazi wa mtaa huo alivyochepusha maji na kuingiza nyumbani kwake kinyume na taratibu. **PICHA: SHABAN NJIA**

## Mafunzo ya amali kutolewa kuanzia ngazi ya sekondari

**Na Rose Jacob,** MWANZA

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, amesema kuwa serikali imekusudia kuanzisha mafunzo ya amali kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne, lengo likiwa ni kuwajengea uwezo na kutambua vipaji vya wanafunzi tangu wakiwa sekondari.

Mkenda alitoa kauli hiyo juzi wilayani Sengerema mkoani Mwanza wakati akikagua eneo la ujenzi wa Chuo Kikuu cha Ardhi, Kampasi ya Mwanza na kueleza kuwa mafunzo hayo yatasaidia kukabiliana na tatizo la ajira.

"Mageuzi ya sasa ya shule ni kuanzia shule za msingi hadi kidato cha nne kutakuwa na mafunzo ya amali, ambayo ni ujuzi, utendaji ufundi, upishi, michezo, uvuvi, ushonaji na kilimo hivyo mwanafunzi akimaliza la saba anakuwa na ujuzi alafu anaendelea na kidato cha nne," alisema na kuongeza:

"..Hivyo akimaliza anaweza kujiajiri mwenyewe katika kazi atakayokuwa na ufanisi nayo zaidi."

Alisema Wilaya ya Sengerema imekuwa ni ya mfano nchini kwa masuala ya kujitolea ujenzi wa madarasa 10 katika Jimbo la Sengerema na Buchosa madarasa saba yaliyojengwa kwa nguvu ya wananchi na kuyafikisha katika hatua ya kupaua.

Mkuu wa Wilaya ya Sengerema, Senyi Ngaga aliwaahidi wananchi kuwa serikali itakuwa nao bega kwa bega katika masuala ya maendeleo, hivyo wasisite kutoa michango ya maendeleo pindi wanapoambiwa hususani masuala ya chakula kwa wanafunzi shuleni na ujenzi wa miundombinu ya maendeleo.

Wakizungumza na Nipashe, baadhi ya wakazi wa Sengerema akiwamo Sendama Shija, waliomba serikali kuharakisha ujenzi wa shule ambazo zimeanzishwa na wananchi ili kuhakikisha wanafunzi wanaotakiwa kuanza kidato cha kwanza mwaka 2024 wasipate taabu wakute madarasa yamekamilika.

# Akamatwa kwa kujiunganishia huduma ya maji kinyemela

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Kahama (KUWASA) imemkamata mkazi wa Mwime Manispaa ya Kahama, Hamisi Omary, akiwa amejiunganishia maji kinyemela na kuisababishia mamlaka hiyo kukosa mapato.

Akizungumza na Nipashe katika eneo la tukio, Ofisa Uhusiano wa Mamlaka hiyo, John Mkama, alisema vitendo hivyo vimekuwa vikihujumu KUWASA na kusababisha kukosa mapato, huku wakihidi kuwachukulia hatua za kisheria wahusika wote.

Alisema mteja huyo alijiunganishia huduma hiyo kupitia chooni na bafuni na kwamba maji yote aliyokuwa akitumia yalikuwa hayapiti kwenye mita ya maji.

Alisema maji hayo yalikuwa yameunganishwa kwa kutumia bomba maalum, kwamba yalikuwa hayapiti katika mita ambayo inatumika kusoma kiwango cha maji mteja alichotumia kwa mwezi, huku akiacha bomba la nje kama gelesha ya kuwahadaa wasoma mita wao.

Hivyo, aliwataka wakazi wa Kahama kutoa ushirikiano kwa mamlaka hiyo katika kuwafichua watu wanaoihujumu kwa kuiba maji, kuharibu miundombinu.

Alisema KUWASA peke yao hawawezi kubaini vitendo hivyo pasipo wananchi kutoa taarifa kwani kuna watu wengine wanaiba vifaa kwa matumizi ya kuuza vyuma chakavu.

Mke wa mtuhumiwa huyo aliyejitambulisha kwa jina moja la Amina alisema alikuwa hafahamu lolote kilichokuwa kinafanywa na mume wake juu ya kuchepusha maji na kuingia chooni akisema tangu ameolewa alikuta mifumo ya maji tayari imeingizwa chooni.

Mmoja wa jirani wa mtuhumiwa ambaye hakutaka jina kutajwa alisema, hawakuwa wanafahamu kuwa jirani yao amejiunganishia maji na badala yake walishangaa kutokumuona akichota maji kwao au katika visima jirani.

Naye Ofisa Mtendaji wa Mtaa wa Mwime Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, Hussein Hamis, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kuwataka wananchi kuacha tabia ya kujiunganishia huduma kinyemela na badala yake wafuate hatua ili waweze kupata huduma kama walivyo watu wengine.




Ukurasa 13

## Watanzania tuwe 'serious' kwa mambo 'serious'!

BUFE

IJUMAA JULAI 7, 2023

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



## Hifadhi Mkomazi na faru adimu mweusi anayelipiwa kwa mkataba

Ukurasa 12

WIKI YA 77 NA BIASHARA

# Rais Samia awafungua macho wana-SADC kilimo kinavyohamia sokoni

**Na Mwandisni Wetu**

SEKTA ya Kilimo nchini imedumu kushika nafasi na ishara endelevu kuwa hivyo nchini, hata kimataifa. Awamu zote tano za uongozi nchini hazijawahi kuiweka kando sekta ya kilimo, mwajiri mkuu kitaifa.

Pia ikizingatiwa leo ni kilele cha sikukuu ya biashara kitaifa maarufu Sabasaba, mahali kilimo kilikofika ni ngumu kukitenganisha na sekta ya biashara, hasa sikukuu hiyo; ina wasifu wote wa kuitwa kilimo cha biashara.

Ni jambo ambalo zama zilizopo za awamu ya sita chini ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan katika harakati zake kuijenga nchi, anaweka bayana kwa kauli na vitendo, dira ni kuuweka Tanzania kuwa katika kilimo biashara.



Vijana walioko kwenye mafunzo ya programu ya BBT katika kituo cha mafunzo cha Bihawana, kilichoanzishwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, wakiwa kazini. **PICHA: MTANDAO**

Ikirejewa awamu ya kwanza ya uongozi nchini, ikitoka mikononi mwa ukoloni, Tanzania ilipokea kilimo na maeneo mengine ya maendeleo katika udhaifu mkubwa na katika kujikomboa, Uhuru na mapambano yakaanza zaidi katika mahitaji ya kujitosheleza kwa chakula, Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere akikibatiza 'kilimo cha kufa cha kupona.'

Katika awamu ya sita iliyopo sasa, chini ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, safari imezama zaidi katika dira kuu mbili; kujitosheleza kwa chakula, vivyo hivyo katika sura ya kibiashara ikiwa ni ajira ya mafanikio.

Hiyo imejionyesha hasa katika bajeti mpya iliyoanza kutekelezwa mwezi huu, ikiwa na uwekezaji mkubwa katika sekta hiyo, ukijumuisha bajeti kuzidishwa maradufu katika msimu wa kilimo uliopo na uliopita mapinduzi ya kuwa na vifaa vya kisasa, ikiwamo umwagiliaji.

Hapo inaendana na kuundwa makambi ya vijana wasomi kuendesha kilimo cha kisasa, ikiwamo mafunzo ya Kilimo chini ya Programu ya BBT katika kituo cha Mafunzo cha Bihawana-,

mkoani Dodoma, zote zikiwa na sura pana kusonga katika kilimo cha biashara, kinachomsaidia mwekezaji, mfanyabiashara na wasio na ajira nchini kujiunga huko; sasa ni dhana zaidi ya kuondokana na njaa.

Ni aina ya mfumo wa kilimo anaouhamasisha Rais Dk. Samia, katika sura ya pili ukiunga mkono maboresho ya kitaalamu kutoka taasisi kongwe za utafiti wa kilimo zilizowekwa kisasa- TARI, katika mengi ikiwamo kubuni mbegu bora na kutafiti ardhi kila kukicha.

Kupitia uzito huo wa kilimo nchini, hivi karibuni Rais Dk. Samia ameweka maelekezo ya kuboresha mfumo wa masoko na utendaji katika mazao kilimo kupitia wizara yake ikiwa sasa kila mkoa kutajengea maghala ya nafaka, kutawanya huduma kitaifa, badala ya kuwapo kwa kanda.

Vilevile Waziri wake wa Kilimo, Hussein Bashe, amaekuwa akifafanua udhibiti wa mauzo holela ya chakula nje ya mpaka, sasa ukiwekewa utaratibu maalum ya kisheria, ikiwamo kuuzwa kupitia mifumo maalum, ili mkulima anufaike sasa na baadaye.

### AJINADI SADC

Wiki hii akifungua mkutano unaohusu wabunge wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, mkoani Arusha, Rais Dk. Samia akasambaza wazo na mikakati yake kwa majirani, akitoa rai kwa nchi wanachama wa SADC kujiwekea mikakati na sera za kuboresha sekta ya kilimo, ikizingatiwa bado zinatajwa kuwa na njaa.

Dk. Samia anasema ni wakati sasa nchi hizo zitumie mikakati na sera hizo ili kuufanya ukanda wa SADC kuwa mzalishaji na msambazaji mkubwa wa chakula Afrika na kwingineko.

Katika mkutano huo wa 53 wa Jumuiya ya Wabunge wa SADC mkoani Arusha, anasema nchi za SADC zina eneo la kilometa za mraba milioni 9.85 zinazofaa kwa shughuli ya kilimo akishauri:

"Kama zitatumiwa vyema, tuna ardhi muhimu kwa ajili ya kilimo, lakini tunapaswa kuhakikisha ardhi hii inazalisha chakula kuziba pengo linalofanya nchi za SADC kuwa na njaa."

Ananadi stadi zake kufikisha biashara kwa majirani zake kwamba matumizi ya sera na mikakati itazaa matunda, akinena: "Tunakuja na sera na mikakati mbalimbali, lakini hatutekelezi, sasa huu ni wakati wa kuzungumza na kuanza kutekeleza."

Dk. Samia anawakumbusha wigo wa soko la kusaidiana kwamba nchi za SADC zina idadi ya watu milioni 380 na takribani asilimia 51.3 wanakabiliwa na njaa, akikumbusha haja ya kutekeleza sera na mikakati inayowekwa kila mara, ikiwamo ya SADC mwaka 2015.

Inaendelea Uk 12

## BIASHARA

# Hifadhi Mkomazi na faru adimu mweusi anayelipiwa kwa mkataba

• Kumpa jina upendalo, picha ya kumbukumbu, kuunda uswahiba...

**Christina Mwakangale na Elizabeth Zaya**

WAKATI Maonyesho ya Sabasaba yakiendelea jijini Dar es Salaam, Mhifadhi Mkuu wake, Happines Kiemi, ambaye ni Mkuu wa Kitengo cha Utalii wa hifadhi hiyo, anapataja kuwa miongoni mwa sehemu zilizopewa hadhi ya kitaifa tangu mwaka 2008.

Hifadhi hiyo inapatikana kwenye mikoa miwili Tanga na Kilimanjaro. Anapataja, njia au milango ya kuingia hifadhini kupitia mikoa hiyo, hupatikana wilaya za Korogwe, Mkinga, Lushoto mkoani Tanga, pia Mwanga, Same kwa mkoa Kilimanjaro.

Anasema kwa sasa hifadhi hiyo imekuja na mbinu mpya ya kuinua kiwango cha watalii na mapato, kwa kubuni utalii maalumu kwa ajili ya mnyama faru, ambaye ni wa kipekee na adimu duniani.

Hifadhi ya Mkomazi, ina ukubwa wa kilomita za mraba 3,245, Happiness akifafanua mgeni anaweza kuingia kwenye malango tofauti yanayowafikisha ndani ya hifadhi hiyo, inayotajwa ya kipekee ikiwa na faru weusi pamoja na wanyama wengine wakubwa watano.

Anafafanua, hifadhi hiyo ina wanyama wakubwa wa aina tano ikiwamo tembo, chui, simba, faru na nyati na kila mgeni mmoja atachagua njia ya kufika hifadhini iwe kwa ndege au barabara.

"Kwa ndege atashuka ndani ya hifadhi na kuruka kwenda hifadhi nyingine," anasema mhifadhi huyo.


Faru mweusi anayepatikana katika Hifadhi ya Mkomazi.

Happiness anasema, njia nyingine ya kufika hifadhini ni kwa kutumia reli mpya anapotoka Dar es Salaam, au hata kwa mabasi kupitia barabara kubwa ya lami, akisifu malazi yapo yanayomilikiwa na shirika hilo na mengine wawekezaji binafsi, ambayo ni kambi kwa kulipia gharama ya kati hadi ya juu.

Anasimulia Nipashe akiwa katika viwanja vya maonyesho ya Sabasaba, Dar es Salaam, Happiness anasema

zipo kambi za muda na zenye madaraja tofauti hata za kisasa maarufu 'luxury.'

"Katika hifadhi ukiwa ndani ukiingia tu kwenye lango, utaona mandhari nzuri za wazi, milima, mabonde na zenye madimbwi ya maji ya asili yanayojaa msimu wa mvua na mengine tunayajaza maji.

"Ukija Mkomazi na 'stress' (msongo wa mawazi), kwa sababu tunaamini mtu anayekuja hifadhini ni kwa ajili ya kupumzika na kuburudika. Hapa utapata huduma kwa asilimia 100 na atatamani kurejea au kuongeza siku za kukaa," anaeleza mhifadhi huyo.

### NDEGE AINA 450

Happiness anasema kwenye hifadhi ya Mkomazi kuna ndege zaidi ya aina 450 na kwamba wakati mtu akiwa ndani ya hifadhi, anauona Mlima Kilimanjaro jinsi jua linavyozama.

"Kwenye hifadhi kuna matukio mengi ambayo hufanyika usiku. Ukiangalia kwenye makala kuhusu wanyamapori katika televisheni utaelewa ninachokisema kwamba wapo wanyamapori ambao wao huwinda usiku, anasema na kuendelea: "Sisi ukija kwetu ukiwa na gari la utalii, utaambatana na askari wa wanyamapori na utaona matukio hayo kwa ukaribu."

Happines anafafanua kwamba, wakati wa utalii kuna wageni wanaofika hifadhini kuwaona ndege hao ambao wengine hutokea bara la Ulaya, msimu wa baridi wakija hifadhi hiyo, wakikwepa baridi la huko.

### MRADI WA FARU

Mhifadhi huyo anasema wakati dunia ikibaini faru ni miongoni mwa wanyamapori ambao wapo hatarini kutoweka, serikali ikawekeza na kuanza kuwalinda kupitia miradi miwili, ikiwamo utalii wa kuwaona faru.

Anasema, mradi huo wa kwanza ulihusisha kuruhusu wageni wa ndani na nje ya nchi, pia ikijumuisha kukaribisha wanafunzi wanaofanya utafiti kwa ajili ya taarifa na kumbukumbu tofauti.

Mradi wa pili, Happiness anautaja wa faru sita weusi, na kwamba mgeni akifika hupewa gari la hifadhi la kitalii na kwenye maeneo yenye misitu, faru hushuhudiwa kwa ukaribu.

"Tulivyoona faru anavutia, tumeanzisha utalii mwingine wa faru kwa mgeni anayependa kumpa zawadi mke wake, mtoto, mume, ana fursa ya kumpa faru jina lolote ambalo analipenda kati ya hao jamaa zake niliowataja, ila atalipia.

"Tunatarajia kuzindua utalii maalumu wa aina nne, ikiwamo kuwapa majina faru maisha yote (Rhino Naming in lifetime), kurekodi matukio (Rhino Capture operation), kurithi (Rhino Adoption) na kuwafuatilia faru (Rhino Tracking).

"Rhino Naming in life time (kulipia jina), italipiwa kwa shilingi miliioni tano na mtalii kutoka nje akilipa dola za kimarekani 5,000.

"Ukimpa jina faru kwa malipo hayo, faru huyo ataitwa jina ulilolitoa kwa maisha yote ya mnyama huyo duniani," anafafanua Happiness.

Anasema lengo la utalii wa aina hiyo, ni kukuza idadi ya watalii wa ndani na nje kwamba kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo idadi ya watalii kutoka nje imeongezeka.

"Tumezoea mtu anampa zawadi, mke, mtoto, wazazi na sisi tumebuni watu waje watembelee hifadhi waende kwenye familia za faru na kuna faru ambao ni yatima wanahitaji kurithiwa.

"Utalii wa 'Rhino Capture Operation' kwa watalii wa ndani shilingi milioni moja na wa nje itakuwa dola 1,000. Pia 'Rhino Adoption' kwa mwaka ni shilingi milioni bili na mgeni kutoka nje ni dola 2,000," anaeleza Kamanda Happiness.

Anasema hifadhi hiyo imekuja na mbinu hiyo ya utalii hususan kwa faru mnyama ambaye yupo kwenye mradi maalumu wa kulindwa: "Kama mtalii atapenda kuungana nasi kwa kufanya 'Rhino Tracking' kwa mtalii wa ndani ni Sh. 500,000 na anayetoka nje ni dola 500. Faru wetu ambao wamefungwa vifaa maalumu wanaweza kufuatiliwa," anaongeza mhifadhi huyo.

"Utalii wa Mkomazi hasa majira ya usiku utaona wanyama ambao hawaonekani mchana na matukio yao ya usiku. Faru mweusi ni adimu ni ambao wameanza kutoweka duniani, serikali iliona umuhimu wa wanyama hao na kuanzisha mradi, ili kuwatunza," anasema

**Kamanda Happiness, anaongeza:**

"Ukienda hifadhi kama Serengeti utawaona kwa mbali faru, ila hawa katika Hifadhi ya Mkomazi utamuona faru chini ya mita moja, ukiwa ndani ya gari la utalii na utaweza kupiga nao selfie (kujipiga picha naye)."


Mnyama anayepatikana katika Hifadhi ya Mkomazi. **PICHA ZOTE: MPIGAPICHA WETU.**

### WAWEKEZAJI WAITWA

Happiness anasema wazawa nchini wanakaribishwa kuwekeza katika Hifadhi ya Mkomazi, kwenye sekta ya utalii hususan maeneo kwa ajili ya malazi na chakula, kutokana na ongezeko la watalii hifadhi hiyo, inayokua kwa asilimia 100.

Ongezeko hilo kwa kipindi cha mwaka mmoja limekua kutoka watalii takribani 3,000 kwa miaka mitatu iliyopita na kufikia 8,000 mwaka huu.

Anasema, kuna ongezeko la haraka la wageni kwenye hifadhi hiyo, hivyo fursa za uwekezaji upo, akisema sababu kuu ya kongezeka watalii ni kufungua utalii wa faru, kuboresha miundombinu ya hifadhi ikiwamo malango ya kuingia hifadhini.

"Mkomazi ina wanyama wote watano wakubwa hifadhini kama vile nyati, faru, simba, chui na tembo, ingawa duma, swala, choroa wapo. Mkomazi ndio hifadhi pekee ambayo unaweza kumuona faru kwa ukaribu.

"Hifadhi hii kwa upekee huo inafanya kuwavutia watalii wengi na kuongeza mnyororo wa thamani wa sekta ya utalii ambao unaweza kumnufaisha kila mwekezaji," anasema mhifadhi huyo.

## Rais Samia awafungua macho wana- SADC kilimo kinavyohamia sokoni

**INATOKA UK. 11**

Rais Dk. Samia anakumbusha kilimo kimekuwa chanzo kikuu cha ajira na kipato kwa watu zaidi ya asilimia 61 ndani ya ukanda wa SADC, hivyo serikali zake zinatakiwa kutilia maanani hilo kufikia malengo yao SADC kuelekea mwaka 2050.

Eneo la nchi za SADC, iko katika kundi la ukanda wenye idadi kubwa ya vijana, hivyo kilimo kinatajwa kuwa na inafasi kubwa ya kutenegeneza ajira zaidi ya milioni 12 ili kuendana na mahitaji hayo.

### KINACHOTEKELEZWA NCHINI

Katika mtazamo huohuo wa kilimo cha kisasa kuelekea kujikimu kwa chakula na biashara, serikali kupitia bajeti ya sasa, 2023/2024 imepanga kufanya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na ujenzi wa Bwawa la Yongoma lililopo wilayani Same, mkoa Kilimanjaro kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na kuinua kipato cha wakulima.

Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, anafafanua hilo akiwataka wana - SADC, kushirikiana kuzalisha chakula kwa mpango ambao kila nchi itanufaika.

Katika kujipanga, Bashe ambaye ni msomi wa biashara, anasema serikali itaendelea kuimarisha ushirika akiamini inaongeza tija katika kilimo kitakachochukua sura ya kibiashara.Hata hivi karibuni, vijana waliopo katika mafunzo ya kilimo chini ya Programu ya BBT katika kituo cha Mafunzo cha Bihawana-Dodoma, wakaishukuru serikali chini ya uongozi wa Rais Dk. Samia Suluhu, kwa kuwafungulia fursa na mwelekeo wa maisha yenye tija.

## TAFAKURI YA MLALAHOI

# Watanzania tuwe 'serious' kwa mambo 'serious'!





**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe:
kulangwasos@gmail.com

VIUMBE hai vyote duniani vina taratibu, desturi, mila na utamaduni wao. Binadamu wanavyo, wanyama wanavyo, bila shaka hata mimea.

Ndiyo sababu binadamu hugombana na kutofautiana, sawa kabisa na wanyama ambao husigana katika masuala ya umiliki wa maeneo au himaya.

Kwa binadamu katika masuala hayo ya mila na desturi, kuna watu wa tabia na nyendo tofauti katika makuzi, na ndiyo sababu wakawamo wakorofi na wachekeshaji.

Katika jamii yoyote ya binadamu, wamo watu wa aina hiyo ambapo kuishi kwao hutegemea zaidi kuchekesha wengine na kufanya utani na masihara.

Kwa njia hiyo, hujipatia umaarufu na hata riziki. Inapotokea hivyo, hakuna anayekuwa tayari kuacha fani yake hiyo, hususan wachekeshaji au waigizaji.

Huo ni mtindo wa maisha ya tangu zama, kwani enzi hizo kulikuwa na wachekeshaji kama Charlie Chaplin na wenzake na ndiyo sababu leo utasikia watu wanatambulishana kuwa huyu ni Chalii wangu.

Wachekeshaji na waigizaji walikuwa na wamekuwa na nafasi kubwa katika jamii, kwani hutumika kama burudani kwa waliochoka na wenye mawazo.

Watu hao wamekuwa kivutio kwa watoto, kwani wamekuwa wakivuta hisia zao kila wanakopita wakichekesha na kutania.

Leo hii katika jamii ya kitanzania, wamewekwa katika kundi la wasanii, wakihusishwa na tamthiliya, futuhi, nyimbo na ngoma.

Tanzania imejaliwa watu wengi wa aina hiyo na wamejizolea sifa kemkem na kutumiwa kwa mambo mengi yakiwamo ya kisiasa.

Mtakumbuka wimbo wa mwanamuziki nguli wa muziki wa dansi, marehemu Ramadhani Mtoro Ongala 'Dk. Remmy' uitwao 'Asili ya Muziki' ambamo katika maudhui yake anasema "mbele ya Mwenyekiti kuhutubia ni muziki huwakusanya watu."

Alitaka kutanabahisha umuhimu wa muziki katika jamii. Na ndiyo sababu hata wasanii aina ya wachekeshaji nao wamekuwa wakitumiwa kwenye mikusanyiko kutoa burudani lakini kubwa kuvuta umati.

Hivyo waliko wasanii aina hii ya wachekeshaji na wapenda kutania, kuna umati wa watu wanaopenda kuburudika na kupumzika baada ya kazi.

Wachekeshaji baadhi yao wamejipatia ukwasi kutokana na kazi zao hizo, mbali na kujizolea umaarufu kwa jamii hata kuaminika kufanya kazi badala au kwa niaba.

Tanzania inapitia kipindi cha malumbano juu ya ushirikiano baina ya serikali yake na ya Dubai, kuhusu uwekezaji kwenye bandari zake.

Malumbano hayo yamejikita katika uwekezaji wenyewe kwa jumla, huku wananchi wakigawanyika misimamo ya ama mwekezaji aje au asije, ama mkataba upite ulivyo au urekebishwe vifungu.

Mgawanyiko huo unaonekana kukosa afya kwa mshikamano wa Watanzania, ambao sasa wamekuwa badala ya kujadili hoja zilizo mbele yao, wananyoosheana vidole.

Kimsingi, hakuna anayepinga maendeleo, hakuna anayepinga uwekezaji, lakini wapo wanaohoji vifungu vya mkataba wa serikali na kampuni ya Dubai Port World (DPW).

Si nia yangu kujadili yaliyomo kwenye mkataba na wala sitaki kujadili upungufu au nguvu zilizo katika mkataba wenyewe, lakini kinachoniliza ni uhusiano wa Watanzania unaovurugwa na malumbano ya mkataba huo.

Sitaki kuingia katika malumbano ya umesainiwa au haujasainiwa, bali kinachoniumiza ni jinsi Watanzania wanavyovunjiana heshima hadharani kwa kitu kinachoweza hata kuondoshwa ikibidi.

Tumefika hatua, wanakosewa heshima watu wenye heshima zao, kama Waziri Mkuu wa zamani na Makamu wa Kwanza wa zamani wa Rais, Mzee Joseph Warioba.

Wanavunjiwa heshima wasomi nguli wa masuala ya sheria, kama Profesa Issa Shivji, kwa sababu tu wamejitokeza kutia maneno wakishauri kuhusu mkataba! Hao ni baadhi tu wapo wengine wengi.

Na badala ya Watanzania kutuliza akili na kukaa chini na kufanya kama ilivyofanyika miaka ya sabini tulipopambana kwa umoja dhidi ya majeshi ya nduli Iddi Amini, tukashinda, tunatafuta nyufa na kuzitanua.

Tunaona sasa ni bora hata kutumia wachekeshaji na waendekeza utani na futuhi, eti kututafutia ukweli wa jambo lilivyo na kuponda wasomi na wataalamu tulionao, kweli?

**Tunaonekana hamnazo kwa kujiingiza katika mpasuko wa udini na siasa, kwa kudhani kuwa ni rahisi kuvunja Muungano na pia kuhasimiana kidini na kudhani kuwa tutabaki salama! Tuwe 'serious' kidogo basi! Alamsiki!**

UCHUMI

# Mkurugenzi Benki Mkombozi aanika ubia na wajasiriamali ulivyowapaisha

**Na Gwamaka Alipipi**

LEO ni kilele cha Sikikuu ya Sabasaba, ambayo inahamasisha na kutathmini mafanikio ya biashara nchini. Daima hilo ni gumu kulifafanua, pasipo kutaja nafasi ya Sekta ya Fedha.

Sekta hiyo kupitia eneo la benki imepitia safari ndefu, kuanzia zama hizo ikitumika kwa teknolojia ya chini, fedha zikihesabiwa kwa mkono.

Kadri muda ulivyobadilika, kama zilivyo sekta nyinginezo kukashuhudiwa mageuzi makubwa. Kuanzia mwanzoni mwa miaka ya 1990, kukapitishwa Sheria ya Fedha nchini na kisha Sheria ya Benki, ambayo ina mageuzi mengi katika sekta hiyo.

Eneo mojawapo ni benki binafsi nyingi zikaundwa, pia kurejea kwa zilizoondoka miaka mingi baada ya Azimio la Arusha mwaka 1967. Yalikuwa ni mageuzi ya kisera nchini.

Kwa mujibu wa sheria inayozisimamia benki hizo, zinapitia awamu mbili katika makuzi yake kulingana na kiwango cha mtaji na uwezo wake kibiashara, kufika hadhi inayoitwa Benki ya Biashara.

Ndani ya zao la mageuzi hayo, ndio inpatikana Benki ya Mkombozi ambayo imemea sasa iko katika hadhi 'Benki ya Biashara' iking'ara katika ufanisi wake.




Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Biashara Mkombozi, Respige Kima. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

### SIRI YA MAFANIKIO

Kama ulivyo usemi 'usione vinaelea vimeundwa; ndio ilivyo kwa Mkombozi yenye makao makuu jijini Dar es Salaam, ikiwa na matawi kadhaa nje ya mkoa.

Mkurugenzi Mtendaji wake, Respige Kima, anaieleza Nipashe kwamba ufanisi wa kiutendaji katika biashara hiyo ya fedha ni matokeo chanya ya utekelezaji wa mikakati ya maendeleo iliyopo na iliyojiwekea.

Anataja katika mwaka wa fedha 2022, chini ya ulezi wa kisheria wa Benki Kuu ya Tanzania, Mkombozi imo katika zilizofanya vizuri kwa kupata faida ya Sh. bilioni 6.79 kwa mujibu wa taarifa za ukaguzi za fedha kwa mwaka huo.

Kima, anasema benki ilipata faida kwa mujibu wa hesabu ya mizania yake, ikiwa ni zao la ufanisi wa utendaji kibiashara na mikakati ya maendeleo waliojiwekea.

"Tulijikita katika fursa za ukuaji wa uchumi wakati tukichukua hatua chanya kukabiliana na changamoto zilizokuwa katika mazingira yetu ya kiutendaji," anaeleza Kima.

Hapo Kima anataja mawili makuu yanayobeba mafanikio ya Benki ya Biashara Mkombozi ni; mapato na gharama za uendeshaji.

"Malengo tuliyojiwekea kwa miaka mitatu iliyopita ni kupanua wigo wa wateja, ambao ni msingi mkubwa wa mapato na ukwasi wa kuendeshea biashara ya benki kwa ufanisi.

"Benki pia iliainisha na kutekeleza mipango mkakati ya kupunguza gharama za uendeshaji kwa ujumla, ikiwa ni pamoja na kuachana na gharama zisizo za lazima," anasema mkurugenzi, akiorodhesha gharama; amana za wateja, pia uendeshaji benki.

"Hivyo tulijikita katika kuongeza wigo wa wateja wetu tuwapate wengi, ili tukusanye amana kutoka kwa wateja wengi, hasa amana za gharama nafuu," anasema Kima.

Anaendelea: "Pia, tulitathmini muundo wa biashara yetu na maeneo ya uendeshaji ambayo yanapaswa kurekebishwa.

"Tulifanya uwekezaji mkubwa kwenye eneo la digitali ili kuleta sokoni huduma ya wakala wa benki na huduma nyingine za digitali kama vile benki kwa njia ya simu, benki mtandao na huduma ya kukusanya mapato kwa mifumo ya kidijitali.

"Tumeendelea kuwekeza katika upanuzi wa matawi yetu ka'ka sehemu mbalimbali za kimkakati kwa benki yetu," anasema.

Anataja kwa katika Mwaka wa Fedha 2022, Mkombozi ilikuwa na salio la mikopo kwa wateja la Sh. bilioni 115 ikiwa ni ongezeko la Sh. bilioni saba kutoka Sh. bilioni 106 mwaka 2021; Pia, anataja salio la amana za wateja kwa mwaka 2022 lilikuwa Sh.bilioni 184 , ambayo ni Sh. bilioni tatu, kutoka Sh. bilioni 181 mwaka 2021.

### HUDUMA ZA WAKALA

Mkurugenzi huyo anasema, Benki ya Mkombozi iliendelea kujikita kimkakati kupanua wigo wa hudima kwa wateja kupitia wakala ambao, kwa takribani mwaka mmoja na nusu sasa, benki imewasajili zaidi ya 400 sehemu nchini kote, akiahidi kuendelea kuboreshwa, hususani vijijini.

Anasema, pia benki hiyo ipo mbioni kufungua matawi kitaifa na mwaka huu imefungua tawi jipya la 12 mkoani Arusha.

### CHANGAMOTO ZILIVYO

Mkurugenzi Kima anabainisha kuwa, wigo mdogo wa wateja ndiyo changamoto kubwa katika ukuaji na ufanisi wa biashara ya benki kwa ujumla.

Ni safari inayohitaji uwekezaji wa muda mfupi kufikia lengo la benki kuwa ya Watanzania wote.

Kuhusu changamoto za wafanyabiashara wadogo, moja ya makundi lengwa ya benki hiyo ni wanaposhindwa kurasimisha biashara zao, akitaja kikwazo kwao ni elimu na utayari wa wajasiriamali kusajili biashara zao, tendo analitraka pia, gharama zake zimekuwa kikwazo.

Kima anasema: "Kuna baadhi ya wafanyabiashara wanakwazika kufanya urasimishaji wa biashara zao, kwa sababu ya gharama za kurasimisha biashara hizo."

Anataja maeneo kama mifumo na taratibu za utoaji wa leseni na vibali, yanahitaji kufanyiwa marekebisho, ili kuleta ufanisi haswa kwa kufupisha muda wa usajili.

Hapo anatoa mfano katika kufungua biashara, kunahitajika lesseni na vibali vinavyotolewa na mamlaka tofauti jambio linalopaswa vyite vitolewe sehemu moja.

Anasema pia elimu ya uwekezaji na uendeshaji wa biashara ni muhimu sana kwa wafanyabiashara wadogo na ni wakati mwafaka kwa taasisi za fedha kuwekeza kwenye elimu ya wajasiriamali, ilikuwaandaa kuwa wateja bora na wa manufaa kwa taasisi hizo na uchumi wa nchi kwa ujumla.

### KUWASAIDIA WAKULIMA

Kima anasema benki nyingi zinazofanya kazi Tanzania za biashara, zina mikakati na malengo yanayojikita kwenye biashara za muda mfupi, zikiangalia vihatarishi vya biashara mbalimbali, hata kufanya biashara mijini zaidu.

"Vihatarishi vya kufanya biashara na mjasiriamali aliyejijenga ni ndogo kuliko yule anayeanza. Hata hivyo benki zinapaswa ziwasikie wajasiriamali wanaoanza kwa kutambua mazingira yao, mahitaji yao na changamoto zinazowasibu, ili kuweza kubuni huduma na mifumo itakayorahisisha na kuwahusisha kwenye huduma za kibenki," anasema.

Anarejea benki yake ya Mkombozi Benki inaangalia makundi ya wajasiriamali wadogo kwa mikopo na huduma nyinginezo.

"Wengi wa wajasiriamali wadogo wanajihusisha na shughuli za kilimo, ufugaji, uchakataji na usambazaji mazao ya kilimo na mifugo; hivyo kwa kulenga kundi hilo, Benki ya Biashara Mkombozi inawezesha sekta ya kilimo katika ngazi ya awali," anasema.

Kwa mujibu wa mkuu huyo, Benki ya Biashara Mkombozi, inatoa mikopo ya wajasiriamali waliojiunda kwenye vikundi vya mikopo ya kuanzia shilingi 300,000 hadi shilingi milioni nne, ziliotolewa katika hatua mbalimbali za ukuaji biashara.

### WASIOKUWA NA DHAMANA

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Kima, wajasiriamali wasiokuwa na dhamana, nao wanahitaji mikopo wanayopewa kupitia vikundi vyao.

Anasema, kwa mwisho wa mwaka 2022 salio la mikopo ya vikundi ilikuwa ni shilingi bilioni 5.8 na kwamba Benki ya Mkombozi imejipanga kuendelea kuwa na wajasiriamali wengi zaidi siku zijazo.

Anasema, kila tawi la Benki ya Biashara Mkombozi, lina sehemu ya mikopo ya vikundi, huduma ambayo imekuwapo kwa zaidi ya miaka mitano sasa.



# Wataalamu kilimo watakiwa kuwasaidia wakulima uzalishaji

**Na Elisante John,** DODOMA

SERIKALI imewataka wataalamu wa kilimo kuongeza juhudi katika kuwasaidia wakulima kuwa na uzalishaji wenye tija.

Mkurugenzi Msaidizi, Huduma za Ugani kutoka Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Upendo Mndeme, aliyasema hayo jana, kwenye ufunguzi wa mafunzo ya kwa wataalamu wa ugani, wakulima na wanahabari, jijini hapa yaliyoandaliwa na Mkulima Mbunifu (MkM) chini ya Taasisi ya Kilimo endelevu nchini (SAT).

"Wataalamu wa ugani tujitahidi sana kuwasimamia wakulima wetu ili wasijutie kilimo wanacholima mkulima alime huku akijua anakwenda kumuuzia nani hasa pale tunaposema tulime kilimo endelevu," alisema.

Naye Ofisa Kilimo Mkuu kutoka TAMISEMI, Hoffu Uwakaje, alitoa rai kwa wataalamu hao kuhakikisha wanakwenda kutoa elimu kwa wakulima juu ya kurudisha rutuba katika ardhi ambayo imechoka kutokana na matumizi bila ya kutumia kemikali.

Awali, akizungumzia mafanikio ya MkM, Erica Rugabandana, alisema kupitia jarida la MkM hivi sasa elimu juu ya kilimo hai imetanuka na kuonesha mwitikio mkubwa kwa wadau wa kilimo nchini.



Meya wa Jiji la Dodoma, Prof. David Mwamfupe (wa pili kulia), akikabidhi nyaraka za kibali cha ujenzi wa kituo cha afya Mkandarasi Selim Constructions Ltd kitakachojengwa eneo la Ilazo, Kata ya Ipagala jijini humo jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Kairuki atoa maagizo kwa maofisa elimu kuhusu ujenzi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Angellah Kairuki, amewaagiza maofisa elimu kusimamia ujenzi wa miundombinu ya shule za msingi na sekondari unaoendelea kwenye maeneo hayo.

Aidha, amewataka maofisa elimu sekondari waliopata magari mapya 51 kuyatumia vizuri ili kuongeza ufanisi na ubora wa elimu kwenye maeneo yao.

Akizungumza jana kwenye hafla ya kukabidhi magari hayo, Kairuki alisema miundombinu hiyo inapaswa kukamilika ili wanafunzi wa kidato cha tano watakaoripoti Agosti 13, 2023 wakute mazingira rafiki. Kuhusu magari, aliwaagiza kuyatumia kutembelea na kukagua shule, kufuatilia maendeleo ya ufundishaji na ujifunzaji pamoja na kushughulikia kero za walimu ili kuleta ufanisi.

"Ni matarajio ya serikali kuwa magari haya yanayogawiwa leo yatakuwa nyenzo muhimu kwa maofisa elimu wetu katika usimamizi na ufuatiliaji wa elimu nchini."

"Tunaamini kwamba hakutakuwa na visingizio kwa ninyi kutembelea na kukagua shule pia kashughulikieni kero za walimu huko shuleni kwao badala ya kuwasubiri wawafuate ofisini," alisema.

Aidha, alitoa rai kwa wakurugenzi wa halmashauri zote nchini kusimamia matumizi sahihi ya magari hayo na kutenga bajeti za matengenezo.

"Serikali inafanya haya yote ili kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020 Sura ya Tatu Ibara ya 78 inayoelezea sekta ya huduma ya jamii kwa upande wa elimu," alisema.

Naye Naibu Katibu Mkuu TAMISEMI anayeshughulikia elimu, Dk. Charles Msonde, alisema kupitia Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo katika Sekta ya Elimu (EP4R) hadi sasa magari 146 yamegaiwa ili kusaidia maofisa hao shughuli za kielimu.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Dennis Londo, alisema magari hayo ni nyenzo muhimu na ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya CCM ya kuweka mazingira rafiki kwa watumishi wa elimu.

# JKT kuanza kupeleka chakula vituo vya kulea watoto

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JESHI la Kujenga Taifa (JKT), limesema kila mwaka sehemu ya mavuno ya mazao ya kilimo ambayo wanalima katika vikosi vyao yatatumika kusaidia katika vituo vya makuzi ya watoto wanaoishi katika mazingira magumu.

Mkuu wa Tawi la Utawala wa JKT, Brigedia Jenerali Hassan Mabena, aliyasema hayo wakati akikabidhi msaada wa mazao kwenye kituo cha makazi ya taifa ya watoto kilichopo Kikombo jijini hapa. Alisema katika makazi hayo mwaka huu JKT limetoa kilo 500 za mchele, kilo 500 za unga, kilo 200 za maharagwe, sukari, juice, mafuta ya kupikia pamoja na mbuzi kama sehemu ya maadhimisho ya miaka 60 ya JKT tangu ianzishwe.

"Tutakuwa tukifanya hili suala kila mwaka JKT pamoja na kazi ya kulinda usalama lakini pia linafanya kazi ya malezi kwa vijana na uzalishaji mali," alisema.

Alisema kila mwaka msimu wa mavuno unapowadia sehemu ya mazao ambayo yanalimwa kwenye kambi za JKT hapa nchini yatakuwa yanapelekwa kwenye vituo hivyo.

"Tutashirikiana pia katika malezi ya vijana na vitu vingine kwa sababu hawa nao ni sehemu ya jamii na JKT pamoja na kazi ya kulinda taifa ni sehemu ya jamii pia," alisema Brigedia Jenerali Mabena.

Aliwataka watoto hao kusoma kwa bidii ili nao waje kuwasaidia wadogo zao wa kituo hicho.

Kamishna Msaidizi wa Ustawi wa Jamii, kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wanawake na Makundi Maalum, Tulo Masanja, alisema kituo hicho kina uwezo wa kulea watoto 250, ambao wanasoma shule za awali msingi na sekondari katika shule mbalimbali.

Alisema ujio wa JKT, katika makao makuu ya kituo hiko kumetoa ushawishi mkubwa kwa watoto hao kusoma kwa bidii ili nao waje kuwa watumishi katika vitengo mbalimbali hapo baadaye.

Hivyo, aliziomba taasisi nyingine kuiga mfano wa jeshi hilo pamoja na kazi za kulinda usalama wa taifa bado wamewakumbuka watoto yatima.

# Waganga tiba asili walalamika utapeli mtandaoni

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAGANGA wa tiba asili na tiba mbadala wamemwomba Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, Camillius Wambura, kuingilia kati kero sita zinazowakabili ikiwamo kutapeliwa mara kwa mara kwa njia ya mtandao.

Akisoma jana risala kwa niaba ya waganga hao, Mussa Daud kwenye mafunzo ya kuinua ubora wa tiba asili na tiba mbadala yaliyoratibiwa na Wizara ya Afya, aliomba jeshi hilo kushirikiana na chama hicho kukomesha matapeli wanaotumia mwamvuli wa tiba asili na tiba mbadala kuwatapeli wananchi.

"Watu wanapokea ujumbe mganga fulani mtumie hela kwa namba hii, matokeo yake tunaonekana watu wa tiba mbadala ni matapeli hii inatuchafulia sifa tunaomba Jeshi la Polisi lishughulikie," alisema.

Aidha, alisema pia waganga hao wamekuwa wakikamatwa ovyo kulingana na mwonekano wao.

Akizungumzia suala la lambalamba, Katibu wa Umoja wa Waganga wa Tiba asili na Wakunga Tanzania (UWAWATA), Lucas Mlipu alisema wao hawatokubali kutumiwa na watu hao kwa manufaa yao wenyewe na kuliomba Jeshi la Polisi kuwa karibu nao ili kuwafichua wahalifu wanaojiita lambalamba.

Naye Mwakilishi wa IGP Kamishna wa Kamisheni ya Polisi Jamii, Faustine Shigolile alikiri kuwapo kwa tatizo la utapeli wa mitandaoni na tapeli mmoja hutuma ujumbe mfupi zaidi ya 30 na humpatia zaidi ya milioni moja na kushauri waendelee kushirikiana kukomesha vitendo hivyo.



# Wakulima watakiwa kupima udongo kabla ya kulima

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKULIMA wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini wametakiwa kupima afya ya udongo kwenye mashamba yao kabla ya kuanza msimu mpya wa kilimo ili kuepuka kutumia gharama kubwa na kupata tija wanayostahili katika uzalishaji wa mazao.

Wito huo ulitolewa jana na Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI) Kituo cha Uyole, Dk. Denis Tippe, wakati wa maonyesho ya kilimo biashara ambayo yalifanyika kwenye mabanda ya taasisi hiyo maeneo ya Uyole jijini Mbeya.

Dk. Tippe alisema kuwa wakulima wengi hawajui afya ya udongo wa mashamba yao, hali inayosababisha watumie gharama kubwa kuendesha kilimo kwenye mashamba hayo huku wakiambulia mavuno kidogo.

"Kwa mkulima kujua afya ya udongo ni jambo la muhimu sana, itawasaidia kujua aina virutubisho vinavyokosekana kwenye udongo na hivyo kushauriwa aina sahihi ya mbolea wanayopaswa kutumia na kupata tija kwenye uzalishaji wa mazao," alisema Dk. Tippe.

Alisema kuwa wakulima wengi ambao hawajui afya ya udongo kwenye mashamba yao hulazimika kununua mbolea nyingi ambayo wakati mwingine haihitajiki kwenye eneo hilo na hivyo kujikuta licha ya kutumia mbolea bado hupata mavuno machache.

Mgeni rasmi kwenye maonyesho hayo alikuwa ni Katibu Tawala Msaidizi wa Uchumi na Uzalishaji Mkoa wa Mbeya, Sid Madito.

Akiwa katika maonyesho hayo alisema kuwa malalamiko ya wakulima kuhusu bei ndogo ya mazao yanatokana na kutofuata ushauri wa wataalamu wakati wa kulima na hivyo kujikuta wanatumia gharama kubwa ambazo zinawalazimu na wao kutaka wauze mazao yao kwa bei kubwa.

Alisema ili mkulima apate faida kutokana na kilimo anachokifanya, ni lazima apunguze gharama za kuendesha kilimo ili anapovuna aweze kuuza mazao yake kwa faida hata kama bei ya soko itakuwa chini.

"Mkulima akizingatia ushauri wa wataalamu, ni wazi kwamba atatumia teknolojia rahisi, mbolea na pembejeo nyingine zitakuwa rafiki na hivyo ataongeza tija ya uzalishaji kwa kupata mazao mengi ambayo hata akiyauza kwa bei ndogo bado atapata faida," alisema Mdito.

Baadhi ya wadau walioshiriki maonyesho hayo walisema kuwa wakulima wanapaswa kuzingatia ushauri huo wa kitaalamu ikiwamo kufanya uchaguzi mzuri wa mbegu hasa zinazostahimili ukame na kutoa mazao mengi ili wapate tija.

Mwakilishi wa Kampuni ya Coteva inayojihusisha na uuzaji wa mbegu bora za mahindi, Torie Mafie alisema uchaguzi wa mbegu kwa mkulima ni muhimu ili aweze kupata mazao bora, mengi na yenye tija.

Alisema mkulima anayetumia mbegu bora anaweza akazalisha mazao mengi na bora zaidi ikilinganishwa na yule ambaye hakutumia mbegu bora na wakati mwingine mbegu bora husababisha mkulima kuwa na mimea imara yenye afya isiyoshambuliwa na wadudu wala magonjwa.

Maonyesho ya kilimo biashara ambayo huratibiwa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI) Kituo cha Uyole hufanyika kila mwaka kwa lengo la kuwafikishia wakulima teknolojia na bidhaa zilizofanyiwa utafiti ili kuongeza tija ya kilimo kwa wakulima.



Mwanzilishi wa Tuzo za Chaguo la Mlaji Afrika (CCAA), Diana Laizer (wa pili kulia), akipeana mkono na Mkurugenzi Mtendaji wa Lake Oil, Abdulrahman Mohamed (wa tatu kushoto), baada ya kampuni hiyo kutangazwa mdhamini mkuu wa CCAA 2023, jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni Furaha Mohamed kutoka Horizon Digital (kushoto), Azmina Mohamed kutoka mgahawa wa Samaki-Samaki (wa pili kushoto) na Mkurugenzi wa Rasilimali Watu wa Lake Oil Juma Nuru. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

## UWT yapokea milioni 6/- ujenzi vyumba vya biashara

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MBUNGE wa Viti Maalumu Mkoa wa Mbeya, Mhandisi Maryprisca Mahundi, amekabidhi msaada wa Sh. 6,000,000 kwa Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT) Wilaya ya Mbeya Vijijini kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa mradi wa vyumba vya biashara.

Mahundi ambaye ni Naibu Waziri wa Maji alikabidhi fedha hizo juzi ikiwa ni mwendelezo wa kutoa Sh. milioni 20 kwa kila wilaya kwa ajili ya ujenzi wa vitega uchumi na kuiwezesha jumuiya hiyo kujitegemea kiuchumi.

Alisema awali alitoa Sh. 5,000,000 kwa ajili ya mradi huo na hivyo kufanya mpaka sasa awe ametoa Sh. milioni 11 na kwamba mpaka kufika Julai 2025 atakuwa amekamilisha ahadi yake yote.

Alisema kila baada ya muda atakuwa anatembelea miradi hiyo kwa ajili ya kufanya tathmini ya utekelezaji kabla ya kutoa fedha zingine za kuendeleza miradi hiyo.

"Namuomba Mungu anisaidie ili mpaka kufikia mwaka 2025 niwe nimekamilisha ahadi yangu ya Sh. milioni 20, mwakani nitakuja hapa kufanya tathmini ya hizi nilizotoa leo," alisema Mahundi.

Aliwataka wajumbe wa UWT katika wilaya zote kuhakikisha wanatembelea miradi wanayotekeleza ili waifahamu na wawe na uwezo wa kuielezea.

Mwenyekiti wa UWT Mkoa wa Mbeya, Edna Mwaigomole, alimshukuru Mahundi kwa kuisaidia jumuiya hiyo kwenye wilaya zote kwa maelezo kuwa kwa muda mrefu jumuiya hiyo ilikuwa inahangaika kupata vyanzo vya mapato.

Aliwataka viongozi wa jumuiya hiyo katika wilaya zote kuendelea kusimamia miradi hiyo ili ikamilike na kuendana na thamani halisi ya fedha zinazotolewa na wadau akiwamo Mahundi.

# Serikali yashauriwa kuboresha miundombinu Hifadhi ya Rungwe

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii, imeshauriwa kuboresha miundombinu ya barabara katika Hifadhi ya Taifa ya Mlima Rungwe ili vivutio vya utalii vilivyomo vifikike kirahisi na watalii ikiwamo katika eneo la Ziwa Ngosi.

Watalii kutoka Zanzibar walitoa ushauri huo juzi walipofanya ziara ya kutembelea Ziwa Ngosi ambapo walishauri pia zijengwe kambi ambazo watalii watakuwa wanapumzika na kulala wanapoendelea na shughuli za utalii.

Mmoja wa watalii hao, Hamad Sagilu alisema eneo la Ziwa Ngosi ni moja kati ya maeneo ambayo yakiboreshwa yanaweza kuvutia idadi kubwa ya watalii na kuliongezea taifa kipato.

Alisema ziwa hilo lina mwonekano wa aina yake ambao ni kama ilivyo ramani ya Bara la Afrika na maji yake yanabadilika rangi jambo ambalo linakifanya kuwa kivutio cha kipekee ikilinganishwa na maziwa mengine.

Alisema ziwa hilo pia ni moja ya maziwa ambayo hayana chanzo cha mto unaoingiza maji wala unaotoa lakini lina mwonekano mzuri unaovutia.

"Kwa hali ya hewa ya hapa tunaamini kwamba pakiboreshwa zaidi itakuwa moja ya maeneo ambayo watalii wengi watakuja, sisi tutawaeleza wenzetu uzuri wa eneo hili na tunaamini wengi watakuja kwa hiyo tunaishauri serikali ijenge hata nyumba za kulala," alisema Sagilu.

Alisema pakijengwa nyumba za kuishi kuna uwezekano hata baadhi ya maharusi wakapafanya kuwa eneo la kufanyia fungate na kuliingizia taifa fedha.

Naye Neshat Nassa Ally alisema hata kama serikali itakuwa haina bajeti ya kujenga nyumba ni vema ikaalika wawekezaji wenye uwezo wakajenga.

Alisema baadhi ya watalii huwa wanapenda wakienda kwenye kivutio chochote waangalie kwa nyakati tofauti ili kushuhudia utofauti wa eneo husika na hivyo akashauri zijengwe kambi ambazo watalii watakuwa wanalala.

Mhifadhi Mkuu wa Mazingira asilia ya Mlima Rungwe, Grace William, alisema katika eneo hilo wanafanya shughuli mbalimbali za kiuhifadhi ikiwa ni pamoja na kuzuia ajali ya moto ili kulifanya eneo hilo kuendelea kuwa na uasili wake.

Alisema kuna eneo ambalo limetengwa kwa ajili ya wawekezaji kujenga miundombinu mbalimbali ikiwemo kambi na maeneo ya watalii kupumzika wakati wanapofanya shughuli zao.

Alisema mpaka sasa serikali imetenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara inayoelekea kwenye eneo la ziwa hilo hasa kufika katika eneo ambalo limetengwa kwa ajili ya wawekezaji.

"Tunaendelea na uboreshaji wa miundombinu kwenye hifadhi hii, hapa tumetenga eneo kwa ajili ya wawekezaji ambao wanauwezo wa kujenga vitega uchumi, wanaweza wakajenga hoteli na maeneo ya kupumzika," alisema Grace.

Aliwataka watalii kutoka maeneo mbalimbali ya ndani na nje kutembelea vivutio vilivyomo ndani ya hifadhi hiyo ili kujifunza mambo mbalimbali ya kiuhifadhi.



## Majaliwa awapa ujanja vijana kuhusu fursa ajira

**NaRahmaSuleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema lugha ya Kiswahili ni fursa nzuri duniani katika kupata ajira, hivyo ni vyema vijana kuichangamkia fursa hiyo.

Aliyasema hayo wakati akizungumza katika ufunguzi wa maadhimisho ya Siku ya Kiswahili yaliyofanyika visiwani Zanzibar.

Alisema Tanzania ni nchi ambayo inatambulika duniani kwa kutumia Kiswahili fasaha na ni lugha inayotumika katika vyuo duniani.

Alisema Kiswahili ni fursa ya kiuchumi hivyo ni vyema wananchi kuitumia fursa hiyo.

Majaliwa alisema Watanzania wana nafasi ya kufundisha katika vyuo mbalimbali duniani lakini kwa bahati mbaya wengi wameshindwa kuitumia fursa hiyo.

Alisema lazima Watanzania wawe mstari wa mbele katika kuitangaza lugha ya Kiswahili na ninafasi ya kutafakari matumizi yake katika nyanja za kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Akizungumzia kuhusu maada zilizojadiliwa katika kongamano hilo ikiwamo udhalilishaji na uchumi wa buluu alisema uchumi wa buluu ni fursa nzuri hasa kwa wanaoishi pembezoni mwa bahari na mito.

Alisema ili Kiswahili kikue lazima kuwe na mkakati na motisha kwa wanafunzi wanaofanya viruri katika lugha ya Kiswahili.

Majaliwa alisema lazima mkakati huo uanze tangu shule za msingi na lazima wizara zenye dhamana kuandaa mpango wa kwenda kufundisha katika nchi mbalimbali.

"Lazima tuenzi Kiswahili ambapo kina maneno mengi yenye kujenga kamusi nzuri," alisema Majaliwa.

Alisema Tanzania inapaswa kuwa chemchemu kwa wanaotaka kuja kujifunza Kiswahili na serikali zote mbili zitahakikisha zinapanua matumizi ya lugha hiyo.

Naye Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Balozi Pindi Chana, alisema huu ni wakati wa Watanzania kukipeleka Kiswahili kimataifa.

Alisema huu ni wakati wa kuona Kiswahili kinasonga mbele kuelekea katika diplomasia ya nchi za SADDC hatua ambayo itasaidia kutengeneza fursa nyingi za ajira kwa vijana.

Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Tabia Maulid Mwita, alisema wameanza kufanyia kazi maagizo yote wanayopewa na viongozi katika mikakati ya kubuni na kukuza Kiswahili.

# Dk. Mwinyi: Undugu wa India, Tanzania tangu enzi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema India imekuwa ikiiunga mkono Tanzania katika sekta mbalimbali za kiuchumi tangu enzi.

Alisema kwa Zanzibar, India imesaidia utekelezaji wa mradi mkubwa wa majisafi na salama ambao unatarajiwa kumaliza tatizo kubwa la upatikanaji wa majisafi na salama katika Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.

Dk. Mwinyi alisema hayo jana, wakati wa mapokezi ya meli ya Jeshi la India ya Majini ya INS Trishul (F43) iliyotia nanga katika Bandari ya Malindi.

Aliipongeza Serikali ya India kwa kuiunga mkono Zanzibar kutekeleza mradi huo uliogharimu zaidi ya Dola za Marekani milioni 91 ambao unakaribia kukamilika.

Alisema India na Zanzibar pia zimesaini mkataba wa maelewano (MoU) wa uanzishaji wa kampasi ya Taasisi ya Teknolojia ya India (IIT) visiwani humo, ambapo Zanzibar itakuwa nchi ya kwanza baada ya India kuwa na chuo cha aina hiyo.

Alisema mbali ya miradi ya maendeleo, India na Tanzania zimekuwa na ushirikiano katika masuala ya ulinzi na kwamba ujio wa meli hiyo unadhihirisha ushirikiano huo.

Dk. Mwinyi alisema Tanzania na India pia zinashirikiana katika masuala ya biashara, hivyo alitumia fursa hiyo kuhimiza ushirikiano zaidi katika eneo hilo.

Waziri wa Mambo ya Nje wa India, Dk. Subrahmanyam Jaishankar, alisema uanzishwaji wa Kampasi ya IIT visiwani humo unadhihirisha mwanzo wa mafunzo ya teknolojia ya India kufanyika nje ya taifa hilo.

Alisema matarajio ya India kwamba uanzishwaji wa Taasisi ya IIT visiwani hapa itachochea upatikanaji wa rasilimali watu wenye ujuzi ambao wanaweza kutumikia nchi yao.

Aidha, alisema ushirikiano wa India na Tanzania hasa Zanzibar umeanza miaka mingi iliyopita ambapo wafanyabiashara kutoka nchi hizo walikuwa wakisafiri kila upande kwa kutumia boti zilizokuwa zikisukumwa na upepo.

Balozi wa India nchini Tanzania, Binaya Srikanta Pradhan, alisema meli ya kijeshi imewasili Tanzania kwa mara ya pili katika kipindi cha miezi tisa hali ambayo inadhihirisha ushirikiano wa kijeshi na usafiri wa majini uliopo kati ya nchi hizo mbili.

Nahodha wa meli hiyo, Kapil Kaushik, alisema meli hiyo ilianza safari yake kutoka Mumbai India miezi miwili iliyopita ikipita katika nchi tano na kusafiri zaidi ya kilomita 18,000 hadi Bandari ya Zanzibar.

Hivyo, alivipongeza vyombo vya ulinzi na usalama vya Zanzibar kwa ushirikiano kufanikisha ujio wa meli hiyo akisisitiza kwamba ni matumaini yake kwamba uhusiano wa India na Tanzania utaendelea kuimarika.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi akisalimiana na Nahodha wa Manowari ya India Ins Trishul, Kapteni Kapil Kaushik, alipoitembelea katika Bandari ya Malindi, Zanzibar jana na kuzungumza na wapiganaji wa Kikosi cha Wanamaji wa India. Katikati ni Balozi wa India nchini, Binaya Pradhan. **PICHA: IKULU**

# Madaktari, wahudumu afya watakiwa kutoa huduma bora

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais, Othman Masoud Othman, amewataka madaktari na wahudumu wa afya kutoa huduma bora kwa jamii.

Aliyasema hayo huko Kizimkazi Dimbani Mkoa wa Kusini Unguja, baada ya kuweka jiwe la msingi katika Kituo cha Afya cha Mama na Mtoto kilichojengwa na wahisani kutoka Oman ikiwa ni juhudi za serikali za kuimarisha upatikanaji wa huduma za afya Zanzibar.

Alisema kwamba kufanya hivyo ni kuonesha kivitendo, kuithamini misaada ya maendeleo inayotolewa na wahisani katika kuunga mkono juhudi za serikali za kuimarisha huduma kwa wananchi wake.

Alisema afya ya mtoto anayeweza kuwa na makuzi bora na akili imara inaanza katika hatua ya kuwapo upatikanaji wa huduma na lishe bora kwa mama na kwamba ni muhimu kwa wahudumu wa afya kujitahidi kuendeleza utoaji wa elimu ya afya.

Alisema kwamba taifa linahitaji vijana wenye siha na afya bora inayotokana na mama kuwa na lishe sahihi na kumnyonyesha ipasavyo mtoto tangu hatua ya awali ya kuzaliwa ili kuijenga misingi ya afya yake kwa mujibu wa taratibu za kitaalamu.

Pia, aliwataka wazazi hasa kinababa kuzingatia ipasavyo muda wa mtoto kupata haki ya kunyonya, maziwa ya mama jambo litakalompa afya bora sambamba na makuzi imara na hatimaye kupata akili bora.

Othman aliwataka wananchi kuacha tabia ya kula sana vyakula vya viwandani kwa kuwa ni miongoni mwa mambo yanayoweza kuleta changamoto kubwa ya afya.

Waziri wa Afya Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui, alisema serikali kupitia wizara hiyo inafanya kila juhudi kuhakikisha kwamba huduma za afya kwa jamii nchini zinaimarika ipasavyo ili kufikia malengo ya dunia.

Alisema kwamba kutokana na hatua hiyo ifikapo Januari mwaka 2024 serikali inakusudia kuifanyia matengenezo makubwa Hospitali ya Rufani ya Mnazimmoja ili kuwa na hadhi na kuwa na kiwango cha kisasa cha utolewaji wa huduma nchini.

Mfadhili wa ujenzi wa kituo hicho kilichogarimu Sh. milioni 77, Mohammed Jamal Alsaid alisema kwamba hatua hiyo ni mwanzo wa mwendelezo wa kuisaidia Zanzibar katika upatikanaji wa huduma kwenye sekta hiyo.




Mkuu wa Kitengo cha Biashara wa Kampuni ya Sukari Kilombero, Fimbo Butallah (kushoto), akijadiliana jambo na Meneja wa Mawasiliano na Uhusiano wa Kampuni hiyo, Willa Haonga katika maonyesho ya 47 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam kwenye viwanja vya Sabasaba, barabara ya Kilwa jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mahakama yawapa haki wakazi 176 waliotakiwa kumpisha mwekezaji

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA Kuu Divisheni ya Ardhi, imeamuru wakazi 176 walioondolewa eneo la Mtego wa Simba Matuga na Kimara, iliyopo Kata ya Kawawa kwa ajili ya kumpisha mwekezaji, Omary Kadri, warudi kwenye maeneo yao.

Mahakama hiyo ilifikia uamuzi huo baada ya kutengua uamuzi uliotolewa na Baraza la Ardhi, Kata ya Visiga na Baraza la Ardhi, Wilaya ya Kibaha iliyotoa amri ya kubomoa nyumba zilizokuwapo eneo hilo.

Februari 2 na Februari 3, mwaka 2023 wakazi wa eneo hilo wa Wilaya ya Kibaha vijijini, mkoani Pwani walivunjiwa nyumba zao zaidi ya 400 na mwekezaji huyo na kuwasababishia kukosa makazi ya kuishi.

Akitoa uamuzi huo, Jaji Lusungu Hemed, alisema mahakama hiyo imepitia majalada, hivyo imebaini uamuzi uliotolewa na baraza la ardhi la kata haukuwa sahihi pamoja na amri zilizotolewa na baraza la wilaya ya Kibaha zimefutwa na kubatilishwa.

"Hakuna jarada wala kesi inayoonesha Kadri ni mmiliki wa eneo hilo na ubomoaji uliofanywa na kampuni ya udalali kwa maagizo ya baraza la ardhi la Kibaha ulikuwa batili hivyo wananchi wanatakiwa kurudi kwenye maeneo yao," alisema Jaji Hemed.

Katika maombi yao, wakazi hao waliwalishwa na wakili, Benitho Mandele, waliiomba mahakama hiyo kama itaridhika ifute maamuzi ya baraza hilo pamoja na amri ya kubomoa nyumba za eneo hilo ifute kwa sababu hayakuwa maamuzi halali.

Pia, walidai kuwa hawajawahi kuhusishwa kwenye usikilizwaji wa kesi yoyote na Kadri anadai ametekeleza hukumu ya mabaraza hao ambalo liliamuru nyumba zaidi ya 400 zibomolewe.

Salum Lubawa na wenzake 175 walifungua kesi ya maombi madogo ya ardhi namba 57/2023 dhidi ya Omary Kadri, Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Bartazar pamoja na kampuni ya udalali ya Adil Auction Mart yakutaka majalada ya kutoka katika mabaraza hayo yapitiwe na mahakama kuangalia usahihi wake.

Hata hivyo, Lubawa akiwa nje ya mahakama alisema wapo kwenye mchakato wa kufungua shauri la madai ya kufidiwa nyumba zao walizovunjiwa.

"Tunaishukuru Mahakama hii imetenda haki tumefungua kesi Aprili, 2023 na maamuzi yameshatolewa leo hii (jana), tunasubiri siku 45 za rufani zikipita tutafungua kesi ya madai ili mali zetu zilizoharibiwa tulipwe," alisema Lubawa.

# Wasiojulikana wachinja wanandoa

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

WANANDOA wakazi wa Kitongoji cha Mwagimagi, Kijiji cha Shilebela, Kata ya Ulewe, Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga, Williamu Manyama na Christina Mahela wanaokadiriwa kuwa na umri kati ya miaka 50-60, wameuawa kwa kukatwa na kitu chenye nchi kali shingoni na watu wasiojulikana.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Kamishna Msaidizi, Janeth Magomi, amethibitisha kutokea kwa tukio hilo katika kitongoji hicho Juni 29 majira ya usiku wakati wawili hao wakiwa wamelala. Linahusishwa na imani za kishirikina.

Alisema kuwa mpaka sasa jeshi hilo linawashikilia watu watatu huku upelelezi zaidi ukiendelea na kuwataka wananchi kuacha tabia ya kujichukulia sheria mkononi kwani kufanya hivyo ni kosa kisheria.

"Taarifa ya tukio hili nilizipata kupitia kwa Mkuu wa Polisi Wilaya ya Kipolisi Ushetu, nikatuma makachelo wangu wakiongozwa na Mkuu wa Upelelezi, walikuta kweli mtu na mkewe wameuawa na mpaka sasa watu watatu wanashikiliwa kwa tuhuma hizo," alisema Magomi.

William Charles ni mtoto wa wanandoa hao waliouawa alisema, tukio hilo lilitokea usiku wakiwa wamelala na hawakusikia kelele katika chumba cha wazazi wake. Asubuhi waliona damu sebuleni ikiwa imeganda na walipoingia chumbani alikuta wazazi wake wamekatwa shingoni.

Alisema ni hali iliyomshtua na kutoa taarifa kwa majirani na walipofika walidai wazazi wao wamechinjwa na kitu chenye nchi kali na wahusika ambao hawajulikani.

Alisema kuwa baadaye alisikia kuna watu wamekamatwa wakihusishwa na tukio hilo lakini mpaka sasa hawafahamu ni kina nani. Anataka hatua zichukuliwe.

Mbunge wa Ushetu, Emannuel Cherehani, aliwataka wananchi kuacha tabia ya kupokea wageni ambao hawawafahamu vyema na badala yake watoe taarifa katika ofisi za vijijini au ofisa mtendaji wa kata ili wawahoji na kujua uhalali wao wa kuingia vijijini. Itasaidia kupambana na matukio hayo.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Mwagimagi, Fabian Vitalis, alisema matukio ya aina hiyo yamekuwa yanatokea mara kwa mara kutokana na eneo hilo kuwa karibu na Hifadhi ya Moyowosi Kigosi. Hakuna kituo cha polisi karibu na eneo hilo.

Alibainisha kuwa hivi karibuni kulitokea tukio la mama kuvamiwa na watu wasiojulikana na kukatwa mapanga na hawakuwapata waliotenda uhalifu.

Matukio hayo yanakinzana na Katiba ya nchi ibara ya 16(1) inayoelekeza "kila mtu anastahili kuheshimiwa na kupata hifadhi kwa nafsi yake, maisha yake binafsi na familia yake na unyumba wake, na heshima na hifadhi ya maskani yake na mawasiliano yake ya binafsi."

Ibara hiyo ya katiba pia inataka serikali kuweka utaratibu wa sheria kulinda haki ya mtu ya faragha na ya usalama na nafsi yake, mali yake na maskani yake.

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA MOROGORO**
**SHERIA YA UMILIKISHAJI WA ARDHI YA MWAKA 1999**
**KUPOTEA KWA BARUA YA TOLEO LA KUMILIKI ARDHI**
**BARUA YA TOLEO YENYE KUMBUKUMBU NAMBA: MMC/LD/14196**
**MMILIKI ALIOANDIKISHWA: AMANI RAJABU KITENGE S.L.P 166 MOROGORO**
**ARDHI: KIWANJA NA. 45 KITALU 'B' MSAMVU MANISPAA YA MOROGORO**
**MUOMBAJI: AMANI RAJABU KITENGE S.L.P 166 MOROGORO**

Taarifa inatolewa **KWAMBA BARUA YA TOLEO LA KUMILIKI ARDHI** iliyotajwa hapo juu imepotea na ninakusudia kutoa **NAKALA HALISI YA BARUA YA TOLEO YA KUMILIKI ARDHI** iwapo hakuna pingamizi litakalotolewa kwa muda wa mwezi mmoja toka tarehe ya taarifa hii itakapotangazwa katika gazeti
**HATI YA BARUA HALISI YA TOLEO** ikionekana, irudishwe kwa **MKURUGENZI WA MANISPAA - MOROGORO** S.L.P 166 MOROGORO

Ambara H.P
KNY: MKURUGENZI WA MANISPAA MOROGORO

**Form No. 2B**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA IRAMBA**
**MAHALI KIOMBOI BOMANI.**
**MAOMBI NA:....13 MWAKA 2023**
**ANNA MRAFA............MUOMBAJI**
**DHIDI YA**
**AMINA ALLY............MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

**KWA: AMINA ALLY WA ILUNDA WA WILAYA YA IRAMBA**
Fahamu kwamba shauri hili limepangwa kutajwa tarehe 20 Mwezi wa 7 Mwaka 2023 saa 2:00 asubuhi mbele ya Mh. B.J. SHUMA Mwenyekiti wa Baraza. Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.
**AMRI** hii imetolewa kwa mkono wangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 28 Mwezi wa 6 Mwaka 2023.

MWENYEKITI

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 19 OF 2023**
**In the Matter of the Estate of the Late GODFREY SALAYA KIVUYO**
**And**
**In the Matter of Application for letters of administration by AUDILIA MNG'ANYA KIVUYO**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN 369 OF 1963)**
All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of administration) is made to the above-named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 04th day of August, 2023.
Dated at Korogwe this 5th day of July, 2023.

**Form No. 2B**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA IRAMBA**
**MAHALI KIOMBOI BOMANI.**
**MAOMBI NA:....08 MWAKA 2023**
**CHRISTINA GUNDA............MUOMBAJI**
**DHIDI YA**
**AMINA MSIKEY ............MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

**KWA: AMINA MSIKEY WA ILUNDA WILAYA YA MKALAMA**
Fahamu kwamba shauri hili limepangwa kutajwa tarehe 20 Mwezi wa 7 Mwaka 2023 saa 2:00 asubuhi mbele ya Mh. B.J. SHUMA Mwenyekiti wa Baraza. Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.
**AMRI** hii imetolewa kwa mkono wangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 28 Mwezi wa 6 Mwaka 2023.

MWENYEKITI

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF RUNGWE DISTRICT**
**AT TUKUYU**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO. 04 OF 2023**
**In the Matter of the Estate of the Late NSAJIGWA ALEX MKAPA**
**And**
**GRACE LEONARD MGANGA.........APPLICANT**

**GENERAL CITATION**
**(Made under rule 75)**
All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 10th day of August, 2023.
Dated at Rungwe this 06th day of July, 2023.

DISTIRCT RESIDENT MAGISTRATE

## Watu 17 wapoteza maisha kuvuta gesi yenye sumu

**JOHANNESBUG,** AFRIKA KUSINI

WATU 17 wamefariki dunia nchini Afrika Kusini, baada ya kuvuja kwa hewa ya gesi ya aina ya nitrate oxide katika migodi ya wachimbaji haramu wa madini.

Maofisa wa eneo hilo walisema watu wengine 15 wamekimbizwa hospitalini kwa ajili ya kupatiwa matibabu, huku watatu kati yao wakiwa mahututi.

Maofisa hao walieleza kwamba hilo linahusishwa na shughuli haramu katika migodi ya dhahabu.

Waathiriwa ikiwa ni pamoja na wanawake na watoto, walikufa baada ya kuvuta gesi hiyo kwenye makazi yasiyo rasmi katika eneo la Boksburg, mashariki mwa jiji la Johannesburg.

Uvujaji huo wa gesi uliotokea Jumatano umehusishwa na uchimbaji haramu wa dhahabu katika eneo hilo.

Gesi ya nitrate oksidi mara nyingi hutumiwa na wachimbaji haramu wa dhahabu wanaojulikana nchini kama zama, kuchujia dhahabu kutoka kwenye udongo ulioibwa kutoka katika mashimo ya migodi yaliyotelekezwa.

Moja ya mitungi ya gesi ilipatikana ikivuja katika mji wa Angelo wenye wakazi wengi.

Waathiriwa walipatikana ndani ya eneo la mita 100 kutoka eneo la tukio.

Hata hivyo, inahofiwa kuna miili zaidi inaweza kupatikana huku timu za uokoaji zikiendelea na kazi yao.

Mkasa huo unakuja miezi sita tu baada ya lori la gesi kulipuka katika mkesha wa Krismasi na kusababisha vifo vya watu 41 katika mji huo. **BBC**

## Wanne wauawa kwa kombora Ukraine

**KYIV,** UKRAINE

WATU wanne wameuawa na wengine tisa kujeruhiwa kufuatia shambulio la roketi usiku wa kuamkia jana kwenye eneo la makazi katika mji wa magharibi mwa Ukraine wa Lviv.

Wizara ya Mambo ya ndani ya Ukraine ilieleza kwamba baada ya tukio hilo shughuli ya uokoaji inaendelea.

Zaidi ya watu saba waliokolewa kutoka kwenye vifusi, huku wengine 60 wakihamishwa kutoka kwenye nyumba zao baada ya kuharibiwa.

Meya wa Lviv, Andriy Sadovyi, alisema kuwa shambulio hilo lilikuwa baya zaidi dhidi ya miundombinu ya raia wa mji huo tangu kuanza kwa uvamizi wa Russia, kufuatia kuteketezwa zaidi ya nyumba 50.

Rais wa Ukraine, Volodymyr Zelensky, aliandika kwenye ukurasa wake wa mtandao wa kijamii wa Telegram kuwa bila shaka kitendo hicho ni shambulio la magaidi wa Russia na litajibiwa. **DW**

# Mkuu wa kundi la Wagner hajulikani alikokwenda

**MINSK,** BELARUS

MKUU wa kundi la wanajeshi mamluki la Wagner, Yevgeny Prigozhin, imefahamika yuko nchini Russia, baada ya siku chache kuripotiwa kwenda Belarus.

Rais wa Belarus, Alexander Lukashenko, alisema kuwa kiongozi huyo ambaye aliongoza uasi wa kutumia silaha kwa muda mfupi nchini Russia, mwezi uliopita hayuko nchini mwake kwa sasa.

Hata hivyo, haijajulikana mahali aliko Prigozhin, na imekuwa kitendawili wapi amehifadhiwa tangu alipoonekana kusini mwa Russia wakati wa maasi.

Chini ya makubaliano ya kumaliza uasi, mashtaka dhidi ya Prigozhin yalifutwa na aliruhusiwa kuhamia Belarusi.

Rais Lukashenko alisaidia kumaliza uasi huo na kuweka mpango wa kiongozi wake kuhamia nchini humo.

Zaidi ya wiki moja iliyopita Rais Lukashenko, ambaye ametawala Belarus tangu 1994, alisema Prigozhin alikuwa amewasili Belarus.

Lakini jana Rais Lukashenko aliwaambia waandishi wa habari kuwa Prigozhin, yuko St Petersburg na hayuko katika eneo lolote la Belarus.

BBC ilifuatilia ndege ya kibinafsi ya Prigozhin iliyokuwa ikiruka hadi Belarus mwishoni mwa Juni, na kurejea Russia jioni hiyo hiyo.

Tangu wakati huo ndege hiyo imefanya safari kadhaa za ndege kati ya mji wa St Petersburg na Moscow, ingawa haijulikani wazi ikiwa Prigozhin alikuwa kwenye ndege. Rais Lukashenko aliongeza kuwa anavyojua wapiganaji wengine wa Wagner bado walikuwa kwenye ngome zao na ambazo zinaweza kujumuisha mashariki mwa Ukraine au kituo cha mafunzo katika mkoa wa Krasnodar nchini Russia.

Kiongozi huyo alisema pendekezo la Wagner kuwaweka wapiganaji wake nchini Belarusi limezitia wasiwasi nchi jirani za Nato.

Alisema haoni kuwa jambo hilo ni hatari kwa Belarus na haamini kwamba wapiganaji wa Wagner wangeweza kuchukua silaha dhidi ya nchi yake.

"Sina wasiwasi kabisa na baadhi ya wapiganaji hapa, kama wanahitaji kuhamasishwa, tutafanya hivyo kwa haraka. Tutaona ujuzi wote walioupata kwenye mstari wa mbele na tutautumia kwa mafunzo yetu," alisema.

Kundi la Wagner ni jeshi la kibinafsi la mamluki ambalo limekuwa likipigana pamoja na jeshi la kawaida la Russia nchini Ukraine.

Uasi wa Prigozhin ulishuhudia mamluki wa Wagner wakivuka mpaka na kuingia Russia kutoka kambi za mashambani nchini Ukraine na kuingia katika mji wa kusini wa Rostov-on-Don, ambao waliteka baadhi ya vituo vya usalama.

Wapiganaji wa Wagner kisha walisafiri kuelekea jijini Moscow na kusababisha Kremlin kuanzisha ulinzi mkali katika mikoa mingi, ikiwa ni pamoja na mji huo mkuu.

Vladimir Putin alishutumu kundi hilo kwa uhaini, lakini chini ya mpango huo uliokomesha maasi hayo, na Prigozhin aliahidiwa usalama na kesi ya jinai dhidi ya Wagner ilifutwa.

Wapiganaji wake waliambiwa wanaweza kusaini kandarasi za kawaida za jeshi, kwenda nyumbani au kuelekea Belarus. **BBC**




Timu ya Uokoaji kutoka kikosi cha usaidizi cha raia wa China, wakijaribu kumwondoa mkazi aliyekumbwa na mafuriko huko Chongqing katika Wilaya ya Wanzhou. Mvua kubwa iliyonyesha iliua watu 15 na wengine wanne wametoweka. **PICHA: EPA-EFE**

# Viongozi wa makabila Sudan walikataa jeshi

**KHARTOUM,** SUDAN

VIONGOZI wa makabila ya Waarabu kutoka eneo la magharibi mwa Sudan la Darfur, wametangaza utiifu wao kwa wanamgambo wa RSF wanaopambana na jeshi.

Wachambuzi wanaonya kuwa tangazo la viongozi hao wa makabila ya Waarabu linaweza kuuzidisha mzozo uliodumu kwa miezi kadhaa sasa na kusababisha vifo vya watu 3000.

Katika ujumbe wa video uliotolewa mapema wiki hii, viongozi hao kutoka makabila saba makuu katika jimbo la Darfur, walihimiza jamii zao kupambana na jeshi badala ya kuwaona wanamgambo wa RSF kama maadui.

Vita kati ya mkuu wa jeshi Abdel Fattah al-Burhan na Mohamed Hamdan Daglo, ambaye anaongoza vikosi vya RSF, vimesababisha maafa katika eneo la Darfur, na wataalamu wanahofia kuongezeka kwa mgawanyiko wa kikabila unaweza kusababisha ghasia zaidi.

Wengi wanahofia kujirudia kwa historia ambayo kundi la wanamgambo wa RSF lenye chimbuko lake kutoka kwa wanamgambo wa kiarabu waliitwa Janjaweed ambao walifanya matukio ya kiatili dhidi ya makabila madogo ya Waarabu huko Darfur kuanzia mwaka 2003. **DW**

HABARI MICHEZO

# PRISONS KUSAJILI SITA, KUINGIA KAMBINI JULAI 15

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Prisons imesema itasajili wachezaji sita tu kwa ajili ya kuongeza nguvu kwenye kikosi chao kwa ajili ya msimu ujao wa Ligi Kuu huku ikipanga kuingia kambini Julai 15.

Akizungumza jana, Msemaji wa klabu hiyo, Jackson Mwafulango, alisema kwa mujibu wa ripoti ya mwalimu Mohamed Abdallah 'Bares', wanahitajika wachezaji sita, huku tayari wakiwa wameshawapa mkono wa kwa heri wachezaji wanne mpaka sasa.

"Tutasajili wachezaji sita, sitotaja majina hapa nitazitaja nafasi zao, beki wa kati mmoja, kiungo mshambuliaji, washambuliaji wawili namba tisa na namba kumi, winga mmoja na kipa mmoja, lakini hii ya golikipa tunasubiri ripoti ya daktari juu ya kipa wetu Musa Mbissa ambaye aliumia kwenye mechi za mwisho za msimu uliomalizika," alisema Mwafulango.

Aidha, alisema kama daktari wa timu hiyo atasema golikipa wao huyo yuko fiti hawatasajili golikipa mwingine .

Pia alibainisha safari hii wanataka kufanya 'pre season' ya nguvu ili kuleta ushindani mkubwa kwenye Ligi Kuu msimu ujao ambayo anaamini kuwa itakuwa ngumu.

"Safari hii kuelekea msimu ujao tunataka kufanya 'pre season' ya nguvu, viongozi wa juu wamesema maandalizi yaanze mapema na tuchague sehemu ya kuweka kambi yetu kwa ajili ya maandalizi hayo," alisema Mwafulango.

Alisema Miji ambayo imetajwa kuwa mmoja wapo watakwenda kuweka kambi ni, Musoma mkoani Mara, Mwanza, Zanzibar au Dar es Salaam.

"Kati ya miji hiyo niliyoitaja, mmoja wapo ndiyo tutaweka kambi, tutaanza Julai 15 na itakuwa ni ya wiki mbili au tatu kabla ya kuanza ligi, kwa sasa kocha Bares yupo mapumzikoni nyumbani kwao Zanzibar, huku Mbeya mazoezi yameshaanza chini ya Kocha Msaidizi, Shaabn Mtupa," alisema.

Tayari Prisons imeshawapa 'thank you' wachezaji Oscar Paul, Ismail Mgunda, Ramadhani Ntobi na Michael Masinda, huku Shaaban Kisiga akipelekwa kwa mkopo kwenye klabu ya Magereza Dar.



Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Mafunzo ya Amali Zanzibar, Dk. Bakari Ali Silima (kushoto), akicheza bao na Mwalimu wa Chuo cha Mafunzo ya Amali Daya Pemba, Juma Mussa Hamad, katika banda la mamlaka hiyo kwenye maonyesho ya 47 ya biashara ya Sabasaba, Dar es Salaam jana. Katikati ni mwalimu wa Chuo cha Mwanakwelekwe, Abdallah Mohamed Ali. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Kagera Sugar yamwinda Mwaipasi

**Na Abdallah Mataka**

KLABU ya Kagera Sugar imeanza harakati za usajili safari hii wakifanya wa kimyakimya baada ya kuelezwa wapo mwishoni kukamilisha usajili wa mshambuliaji wa Mbeya City, Gasper Mwaipasi aliyeachana na timu hiyo baada ya kushuka daraja msimu uliomalizika.

Katibu Mkuu wa timu hiyo, Ally Masoud, alisema mazungumzo na wachezaji ambao wanataka kuwasajili yanaendelea vizuri hivyo amewataka mashabiki wa timu hiyo kuachia kamati ya usajili kufanya kazi yake.

Masoud aliongeza kuwa wanafanya usajili kwa kufanyia kazi ripoti ya kocha wao, Mecky Mexime katika kufanyia kazi mapungufu ambayo yamejitokeza katika msimu uliomalizika.

"Usajili wetu sio wa mbwembwe kama timu nyingine ndio maana huoni tukihusishwa sana kwa sababu mambo yetu tunafanya kwa utaratibu mzuri na umakini zaidi," alisema.

Ally Masoud alisema licha ya wengi kuona ukimya wao ila haina maana kwamba hawajasajili mchezaji yeyote isipokuwa wanachokifanya ni kukamilisha dili hizo mapema iwezekanavyo ili ibaki kazi ya kuwatangaza tu kwa pamoja wachezaji hao.

"Tunaendelea na usajili kama ilivyokuwa utaratibu wa kipindi hiki, wapo ambao tumefikia makubaliano lakini wengine bado tunaendelea na mazungumzo na yatakapofikia sehemu nzuri watakuwa sehemu ya kikosi chetu kwa msimu ujao," alisema.

Aidha Masoud alikataa kutaja majina ya wachezaji ambao tayari imewasajili mpaka hivi sasa huku akiwataka wapenzi na mashabiki wa timu hiyo kuwa na subira kwani mpango wao ni kuwatambulisha wachezaji hao wote kwa pamoja baada ya kukamilika kwa sajili zao hizo ili kuja kuongeza nguvu katika kikosi hicho cha wana Super Nkurukumbi kutoka Misenyi mkoani Kagera.

"Kuhusu Mwaipasi nadhani mashabiki wasubiri kauli ya klabu juu ya usajili, kama yupo kwenye orodha ya wachezaji tunaowataka watasikia na watamwona," alimaliza kusema Masoud.

## New Generation, JKT Queens uso kwa uso

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MABINGWA wa soka la wanawake Zanzibar na Tanzania Bara, New Generation na JKT Queens zimepangwa kundi moja kwenye michuano ya mchujo kuwania kufuzu fainali za klabu bingwa Afrika kwa ukanda wa Afrika Mashariki.

Katika droo iliyofanyika juzi Jumatano nchini Morocco timu hizo zimepangwa kundi B pamoja na Vihiga Queens ya Kenya na AS Kigali Womens kutoka Rwanda.

Michuano hiyo ya kufuzu fainali za Afrika kwa wanawake imepangwa kuanza Agost 12 mpaka Agosti 30, mwaka huu nchini Uganda.

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), New Generation Queens itatupa karata yake ya kwanza dhidi ya mabingwa wa Kenya timu ya Vihiga Queen's Agosti 12 na siku inayofuata JKT Queens wataumana na AS Kigali Women.

Akizungumza na Nipashe Meneja wa New Generation Queens, Farid Hamza, alisema wanaendelea na maandalizi ya kuelekea michuano hiyo ambayo amesema ni michuano migumu.

Alisema michuano ambayo inakutanisha mabingwa wa nchi zao haiwezi kuwa rahisi hivyo wanahitaji kufanya maandalizi makubwa.

## Shija awashukuru wadhamini kumwandaa

**Na Saada Akida**

BINGWA wa mchezo wa Muay Thai, Emmanuel Shija, amewashukuru wadhamini wake Stephan's Pest Store kwa kudhamini kambi yake ya maandalizi kuelekea kwenye pambano lake la kuwania mkanda wa Ubingwa wa Dunia wa WBC litakalopigwa Julai 19, mwaka huu, jijini Dar es Salaam.

Shija atapanda ulingoni kwenye pambano hilo dhidi ya Yusuf Fundi katika pambano litanalotarajia kupigwa kwenye Ukumbi wa Super Dome uliopo Masaki.

Siku hiyo pia kutakuwa na pambano la bingwa wa WBA -Asia, ambapo Abdul Ubaya atapanda ulingoni kupigana na Ivan Somba wa Uganda katika pambano ambalo limepewa jina la Bongo Fight Championship.

Akizungumza na Nipashe jana, Shija alisema anawashukuru wadhamini wake wa Stephan's Pets Store kwa kuweza kudhamini kambi ya maandalizi ya pambano lake hilo.

"Nawashukuru sana Stephan's Pets Store kwa kuweza kudhamini kambi yangu katika kipindi cha mwezi mzima kuelekea katika pambano langu dhidi ya Yusuf Fundi ambaye tutapigana kuwania mkanda wa WBC Muyai Thai kwa mara ya kwanza Tanzania ingawa kutakuwa na mapambano mengine ya mchezo wa ngumi za kulipwa.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**KANE NA SPURS**
KLABU ya Tottenham Hotspur imempa mshambuliaji wa England, Harry Kane mwenye umri wa miaka 29, ofa ambayo itaboresha sana mshahara wake wa sasa wa pauni 200,000 kwa wiki akiamua kubaki katika klabu hiyo. **(Guardian)**

**TUCHEL AKUTANA NA KANE**
KOCHA wa Bayern Munich, Thomas Tuchel amekutana na Harry Kane nyumbani kwake huku klabu hiyo ya Ujerumani ikijaribu kumsajili mchezaji huyo. **(Bild, via Mail)**

**MILAN NA PULISIC**
AC Milan imewasilisha ofa iliyoboreshwa ya pauni milioni 24 kwa ajili ya winga wa Chelsea na Marekani, Christian Pulisic mwenye umri wa miaka 24. **(Mail)**

**MAN YAKOMAA NA ONANA**
KLABU ya Manchester United inatayarisha dau la pauni milioni 39 kwa ajili ya mlinda mlango wa Inter Milan raia wa Cameroon, Andre Onana mwenye umri wa miaka 27. **(Fabrizio Romano)**

**TIMBER ATUA ARSENAL**
ARSENAL imefikia makubaliano ya pauni milioni 38.5 na Ajax kwa ajili ya beki wa Uholanzi, Jurrien Timber mwenye umri wa miaka 22. **(Standard)**

**ARSENAL PAUNI MIL 200**
ARSENAL watatumia hadi karibu pauni milioni 200 ya bajeti yao ya majira ya joto baada ya kuafikiana na Jurrien Timber na kiungo wa kati wa West Ham, Declan Rice mwenye umri wa miaka 24. **(Telegraph)**

**BARNES ANUKIA NEWCASTLE**
KLABU ya Newcastle United inaongoza katika kinyang'anyiro cha kumnunua kiungo wa kati wa Leicester City na England, Harvey Barnes mwenye umri wa miaka 25, huku Aston Villa na Tottenham Hotspur pia zikimwania. **(Guardian)**

**CAICEDO OFA MPYA**
CHELSEA inatayarisha ofa ya pauni milioni 85 kwa kiungo wa kati wa Brighton na Ecuador, Moises Caicedo mwenye umri wa miaka 21. **(Diego Arcos, via Football.London)**

**LAVIA AVUTIWA**
CHELSEA pia inavutiwa na kiungo wa kati wa Southampton raia wa Ubelgiji, Romeo Lavia mwenye umri wa miaka 19. **(Sky Sports)**

**MOUNT ALIKATAA**
MCHEZAJI mpya wa Manchester United, Mason Mount mwenye umri wa miaka 24, alikataa ofa ya kulipwa mshahara wa pauni 200,000 kwa wiki na Chelsea wakati ikijaribu kumbakisha kiungo huyo wa kati wa England pale Stamford Bridge. **(Athletic)**

**COLWILL ATAKIWA LIVER**
LIVERPOOL inavutiwa na mlinzi wa England, Levi Colwill mwenye umri wa miaka 20, ambaye Chelsea bado wanahitaji huduma yake. **(Football.London)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# RAIS PSG AMTAKA MBAPPE ASAINI MKATABA AU AONDOKE

Klabu hiyo haitaki kumwona anaondoka kama mchezaji huru baada ya mkataba wake kuisha...

**PARIS, Ufaransa**

MSHAMBULIAJI wa Paris Saint-Germain, Kylian Mbappé lazima asaini mkataba mpya ikiwa anataka kubakia katika klabu hiyo, kwani mabingwa hao wa Ufaransa hawatamruhusu kuondoka bure mwakani, rais wa klabu hiyo, Nasser Al-Khelaifi amesema.

Mbappé alituma barua kwa PSG mwezi uliopita ikisema kwamba hana nia ya kuongeza mkataba wake ambao unamalizika mwaka 2024.

Lakini baadaye alifafanua kwamba hakuiomba klabu hiyo ya Ufaransa imruhusu kuhamia kwa miamba ya Hispania, Real Madrid, ambayo siku za nyuma ilijaribu na kushindwa kumpata fowadi huyo aliyeshinda Kombe la Dunia mwaka 2018.

PSG wanakabiliwa na tatizo la kumpoteza Mbappé bure kama hatasaini mkataba mpya msimu huu wa joto na hivyo watakuwa wameingia hasara ya kushindwa kurejesha kitita cha euro milioni 180 walichotumia mwaka 2017 kumsajili kutoka AS Monaco.

"Msimamo wangu uko wazi sana. Sitaki kurudia kila mara; kama Kylian anataka kubaki anatakiwa kusaini mkataba mpya," alisema Al-Khelaifi akiwaambia waandishi wa habari baada ya kumtambulisha Luis Enrique kama kocha mpya wa klabu hiyo.

"Hatutaki kumpoteza mchezaji bora zaidi duniani kwa uhamisho wa bila malipo -- hatuwezi kufanya hivyo. Hii ni klabu ya Ufaransa.

"Hataondoka bure. Ikiwa atabadilisha mawazo yake leo, sio kosa langu. Hatutaki kumpoteza mchezaji bora wa dunia bure, hilo liko wazi."

Mbappé alimaliza kama mfungaji bora wa Ligue 1 katika misimu mitano iliyopita, na PSG watakuwa na nia ya kumbakisha, wakiwa tayari wamempoteza Lionel Messi kwa uhamisho wa bure.

Messi, mshindi wa Ballon d'Or mara saba, aliamua kutoongeza mkataba wake na kuhamia Inter Miami.

# DI MARIA ARUDI KLABU YAKE YA KWANZA ULAYA



**LISBON, Ureno**

MAISHA ya Angel Di Maria barani Ulaya yameingia kwenye mzunguko mwingine baada ya winga huyo kuamua kujiunga tena na Klabu ya Benfica ya Ureno akiwa mchezaji huru.

Di Maria katika maisha yake ya kwanza kucheza soka Ulaya alisajiliwa na Benfica ambako aliichezea kati ya mwaka 2007 na 2010.

"Karibu nyumbani, Di Maria!" Klabu hiyo ilisema baada ya video iliyotangaza kusajiliwa kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 35 ambaye kwa mujibu wa ripoti, amekubali kusaini mkataba wa mwaka mmoja.

Katika maisha yake ya kwanza Di Maria Ulaya akiwa na mabingwa hao wa Ureno ndio yaliyomfanya kuonwa na wababe wa Hispania, Real Madrid.

Alijiunga nao ambako alishinda nao taji la ligi, mataji mawili ya ndani na Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Muargentina huyo alikaa msimu uliopita akiwa na Juventus ya Ligi Kuu Italia, Serie A, baada ya miaka saba ya mafanikio akiwa na Paris Saint-Germain.

Di Maria huko Ureno ataungana na rafiki yake wa karibu, Nicolas Otamendi raia mwenzake wa Argentina ambaye walishinda nae kombe la Dunia.

# Milan yatuma ofa mpya kwa Pulisic

**MILAN, Italia**

AC Milan imewasilisha ofa mpya yenye thamani ya zaidi ya euro milioni 20 kwa mshambuliaji wa Chelsea, Christian Pulisic, kwa mujibu wa ESPN.

ESPN iliripoti wiki iliyopita kwamba Pulisic alikubaliana nao maslahi binafsi na Milan, ambapo nyota huyo wa Marekani anataka kucheza kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

Vyanzo viliiambia ESPN kwamba, Milan wana uhakika wa kufikia makubaliano na Chelsea juu ya ada ya uhamisho, huku klabu hiyo ya Italia ikiamini kwamba



akiba ambayo Chelsea ingeweka kwenye mshahara wa Pulisic kama euro milioni 15 kwa mwaka inatosha kupata makubaliano ya ofa yao mpya.

Klabu ya Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, Lyon pia imeonesha nia ya kutaka kumsajili Pulisic.

Lakini mshambuliaji huyo alikataa ofa kutoka klabu hiyo, akiamini kuwa ni hatua mbaya katika maisha yake ya soka.

Pulisic alijiunga na Chelsea kwa uhamisho wa euro milioni 64 kutoka Borussia Dortmund mwaka 2018 na amefanikiwa kucheza mechi 145 katika misimu minne katika klabu hiyo.

# Man United yamvalia njuga Onana

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United imeiambia Inter Milan kwamba iko tayari kutoa pauni milioni 40 kwa mlinda mlango wao, Andre Onana, kwa mujibu wa ESPN.

Mazungumzo na wawakilishi wa Onana yaliyoanza wiki iliyopita, yamekuwa na tija na United iko tayari kutoa kiasi kinachotakiwa na Inter pamoja na nyongeza.

Vyanzo viliiambia ESPN kwamba hesabu ya Inter ni zaidi ya pauni milioni 50, lakini kuna matumaini kwamba maelewano yanaweza kufikiwa.

Timu hiyo ya Serie A inafahamu nia ya Onana kuhamia Old Trafford, ambako ataungana tena na kocha wake wa zamani kule Ajax, Erik ten Hag.

Ten Hag amemtambua mchezaji huyo wa kimataifa wa Cameroon kama shabaha yake anayopendelea zaidi inapotafuta kipa mpya msimu huu wa joto.

Vyanzo viliiambia ESPN kwamba United bado inaendelea na mazungumzo ya ana kwa ana na David de Gea kuhusu hali ya mkataba wake. Mkataba wa De Gea uliisha Juni 30 na sasa ni mchezaji huru.

Dean Henderson amekuwa akifanya mazoezi pale Carrington wiki hii baada ya kumalizika kwa muda wake wa mkopo kule Nottingham Forest.

Vyanzo viliiambia ESPN kwamba Forest inataka kumsajili Henderson kwa mkataba wa kudumu na, kwa jinsi mambo yanavyoendelea, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 ana uwezekano mkubwa wa kuwa sehemu ya kikosi cha United kwa ajili ya ziara ya kujiandaa na msimu mpya nchini Marekani, itakayoanza New York Julai 20.

Henderson amebakiza miaka miwili kwenye mkataba wake, lakini amedhamiria kutaka kupigania nafasi kwenye kikosi cha kwanza katika juhudi za kurudisha nafasi yake kwenye kikosi cha timu ya taifa ya England.

Tom Heaton mwenye umri wa miaka 37, ndiye kipa mwingine pekee mwandamizi pale United baada ya kuongeza mkataba wa mwaka mmoja mwishoni mwa msimu uliopita.

United walizindua usajili wao wa kwanza wa majira ya joto Jumatano kwa kumnasa kiungo Mason Mount kutoka Chelsea kwa pauni milioni 55 na amepewa jezi namba 7 hapo Old Trafford.

# KOCHA WA AZAM AIBUKIA SIMBA, ONANA ACHAMBULIWA RWANDA

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imemtambulisha kocha wa zamani wa makipa wa Azam FC, Daniel Cadena kuwa mwalimu wa magolikipa wa timu hiyo kwa mkataba wa miaka miwili.

Taarifa iliyotolewa jana na klabu hiyo, inasema kuwa Cadena (45), anakuwa kocha wa makipa wa timu hiyo, akichukua nafasi ya Mmorocco, Zakaria Chlouha ambaye alipewa 'thank you' hivi karibuni baada ya kudumu kwa takriban miezi sita tu.

Mbali na Cadena, pia Simba imemtangaza kocha wa viungo, Corneille Hategikimana raia wa Rwanda kutoka klabu ya As Kigali ambaye amesaini mkataba wa miaka miwili kuitumikia timu hiyo.

"Uongozi wa Simba umefikia makubaliano kumwajiri Daniel Cadena kuwa kocha wa makipa kwa mkataba wa miaka miwili.

Cadena, amejiunga na Simba akitokea Azam FC alipodumu kwa mwaka mmoja na ana leseni ya UEFA na uzoefu mkubwa," ilisema taarifa hiyo.

Kocha huyo raia wa Hispania alikuja nchini na kujiunga na Azam, Juni mwaka jana na amedumu hadi msimu ulipoisha, lakini akawa mmoja kati ya watu wa benchi la ufundi lililoondolewa .

Wakati huo huo, Mwandishi wa Habari za Michezo nchini Rwanda, Gakuba Abdul Jabar ameipongeza Simba kwa kunasa saini ya winga na kiungo mshambuliaji Willy Essomba Onana, raia wa Cameroon, akisema atawasaidia sana kwa kuwa ni mchezaji mzuri.

Gakuba amesema kwa uzoefu wake wa kazi hiyo kwa miaka 18, ameona wachezaji wengi nchini Rwanda, lakini Onana ni mmoja kati ya wachezaji wachache bora aliowashuhudia.

"Niseme Simba imelamba dume ni kijana mwenye uwezo mkubwa, anaufundi wa hali ya juu, hasa timu ikiwa na umiliki, ndiyo utaweza kuona ubora wake, kwa sababu akiwa na mpira hakuna mchezaji au beki anaweza kumsumbua, ana uwezo wa kumhadaa beki na kumpita na ana kasi kubwa hasa akiwa ndani ya eneo la hatari, akipata nafasi mbili tatu ni lazima atapachika bao," alisema mwandishi huyo akiwa nchini Rwanda.

Hata hivyo amesema mabao yake mengi anayafunga akiwa ndani ya eneo la boksi eneo ambalo ndiyo huwa hatari zaidi.

"Siyo mchezaji anayepata nafasi anakosakosa ovyo, kwa sababu ni mchezaji ambaye anafikiri haraka sana, anajiamini akiwa na mpira, kusema kweli sina mashaka na uwezo wake, na mabao yake mara nyingi anayafunga akiwa ndani ya boksi, lakini kingine anasaidia sana wengine kufunga, hana uchoyo, akiona mchezaji mwenzake yupo eneo ambalo anaweza kufunga bao.

Akizungumzia mashaka ya baadhi ya mashabiki wa soka Tanzania kuwa ana majeraha ya mara kwa mara, amesema si kweli badala yake alisumbuliwa na tatizo hilo mzunguko wa kwanza wa msimu wa kwanza wakati anaingia akitokea nchini kwao Cameroon.

"Msimu wake wa kwanza alisumbuliwa na majeraha kidogo, lakini msimu wa pili ndiyo akawa bora zaidi, nafikiri awali hakuwa na utimamu wa mwili, lakini alipoanza kuwa na fiziki alipachika sana mabao, naamini angekuwa na utimamu wa mwili msimu wote, Rayon Sport ingeweza kuwa Mabingwa wa Rwanda," alisisitiza.

Onana alimaliza ligi akiwa mfungaji bora msimu uliomalizika, akipachika mabao 16 na 'assist' 5, lakini akiwa ndiye mchezaji bora wa msimu.




Marais Samia Suluhu Hassan (kulia) na Lazarus Chikwera (wa pili kushoto), wakiwa wameshika jezi mpya za Yanga baada ya kukabidhiwa na rais wa klabu hiyo, Injinia Hersi Said (katikati) Ikulu ya Malawi juzi. **PICHA: BINZUBEIRY**

# Jezi Yanga zagombewa Dar es Salaam

**Na Saada Akida**

SIKU moja tu baada ya kuzinduliwa rasmi jezi mpya za klabu ya Yanga kwa ajili ya msimu wa 2023/2024 mamia ya mashabiki wa timu hiyo wamejitokeza kwa wingi kununua na kuzifanya kuwa adimu.

Yanga wamezindua rasmi jezi zao juzi usiku nchini Malawi kwenye Ikulu ya nchi hiyo ambapo klabu hiyo imepata mualiko na kucheza mechi moja ya kirafiki dhidi ya Nyasa Big Bullets.

Jezi hizo zilizinduliwa mbele ya Marais Dk. Samia Suluhu Hassan na Rais wa Malawi, Lazarus Chakwera katika hafla iliyofanyika Ikulu ya Malawi ambapo Yanga ilialikwa kwa ajili ya mchezo maalum kuadhimisha siku ya uhuru wa nchi hiyo.

Wakati uzinduzi wa jezi hizo ukifanyika Malawi, hapa nchini mamia ya mashabiki wa klabu hiyo walijitokeza kwa wingi kwenye maduka mbalimbali jijini Dar es Salaam likiwamo duka la klabu hiyo lililopo kwenye jengo la Makao Makuu ya klabu hiyo.

Mwandishi wa habari hii alishuhudia jezi hizo zilianza kuuzwa saa 12:00 asubuhi katika duka la klabu hiyo na jezi zilizokuwa zikigombaniwa ni zile zenye rangi nyeusi na ufito wa njano.

Mmoja wa mashabiki waliojitokeza kununua jezi hizo aliiambia Nipashe kuwa jezi za msimu huu zimewavutia zaidi kutokana na ubunifu wake.

"Mimi nilianzia Kariakoo kule nikakuta watu wengi jezi chache na niliyokuwa naitaka hii nyeusi zilikuwa hakuna, nimekuja hapa klabuni napo watu wengi na wengi wanazitaka rangi hii nyeusi," alisema Abdallah Kombo mkazi wa Kimara.

Shabiki mwingine Joseph Kamili alisema alifika klabuni hapo saa 6:00 mchana na kukuta jezi rangi anayoitaka hakuna na kuamua kwenda kuitafuta maduka ya Kariakoo.

Kwa mujibu wa ofisa habari wa Yanga, Ali Kamwe aliiambia Nipashe kuwa jezi zao zimeingia katika rekodi ya kuzinduliwa ndani ya Ikulu na Marais wawili wa nchi tofauti.

Alisema jezi hiyo imezinduliwa kwenye Ikulu ya Malawi mbele ya marais wawili akiwamo rais wa Tanzania, Mama Samia.

"Huu ndio ukubwa wa Yanga, jezi zetu zimetambulishwa ndani ya Ikulu ya Malawi, ni jezi kali ambayo mwanayanga yeyote atajivunia kuwa nayo, kwa viongozi wetu wa klabu tayari Makamu wetu wa Rais, Arafat Haji ameshachukuwa jezi yake na kuweka namba 6 mgongoni," alisema Kamwe.

## Wakongwe Simba, Yanga wataka wachezaji wazawa kujitambua

INATOKA UK. 24

Yanga zinafanya vizuri kwenye mashindano ya kimataifa wachezaji wazawa walipaswa kutumia nafasi hiyo kusaka timu kubwa nje ya Tanzania.

"Timu zetu zinaenda nje, zinafanya vizuri mashindano yakiisha timu kubwa za Afrika zinakuja kuchukua wachezaji, lakini cha kusikitisha wachezaji waokwenda huko ni wa kigeni na wachezaji wetu wanabaki kwenye ligi yetu, ni lazima mchezaji uwe na malengo na kuacha kubweteka, kujituma ni muhimu lakini lazima mchezaji ujitambue," alisema.

Kwa upande wake winga na kiungo mshambuliaji wa zamani wa Yanga, Sekilojo alishangaa kuona kwa sasa Tanzania hakuna mshambuliaji hatari kwenye ligi tofauti na zamani ambapo karibu kila timu ilikuwa nao mmoja au wawili.

"Yaani humwoni mchezaji hatari katika nchi, ukiangalia kwenye ligi yetu sasa hivi mfungaji bora ni Fiston Mayele wa Yanga na Saido Ntibazonkiza wa Simba, wote hawa ni wageni, kuna haja ya wachezaji wetu kujiangalia sana na kufanya mikakati ya kujirudisha kuwa kwenye levo hiyo ambayo si ya kucheza ligi tu, ila kupata nafasi ya kucheza na kuonyesha uwezo na hatimaye kuwatambulisha kwenye mataifa mengine," alisema mkongwe huyo.

Alisema, wachezaji wa kitanzania kama wataamua kucheza soka la malengo wanaweza kufika mbali kwa sababu sasa hivi wanapata fursa nyingi za kujulikana nje ya mipaka ya Tanzania tofauti na kipindi chao.

## Hatima ya Mayele Yanga kujulikana J'3

INATOKA UK. 24

Alisema anacheza mpira kutafuta pesa na ana familia inayomtegema hivyo lazima maamuzi yake yawe sahihi.

"Hata kama nitaondoka Yanga basi nitapata baraka zote kutoka kwa viongozi wangu, kama itatokea tofauti na hilo yote sawa kwa sababu mimi sipendi fujo na nimeishi na Yanga vizuri," alisema Mayele.

Kuhusu Meneja wake, Jasmin Razack alisema hawezi kumwingilia katika maamuzi yake licha ya kumshauri na kumwongoza katika mambo mengi ya mpira.

"Kuna mengi yanaongelewa kuhusu Meneja wangu niweke wazi tu mwenye maamuzi ya kuondoka ni mimi na sio yeye, hakuna shida kati ya Jasmin na uongozi wa Yanga, wanakutana na kuzungumza vizuri juu ya hatima yangu," alisema Mayele.

Michezo

Ijumaa Julai 7, 2023

Nipashe



**Rais PSG amtaka Mbappe asaini mkataba au aondoke** UKURASA 21



Mchezaji wa Yanga, Sharif Kimbowa, akiruka juu kuwania mpira katikati ya mabeki wa Nyasa Big Bullets wakati wa mchezo wa kirafiki wa kuadhimisha miaka 59 ya Uhuru wa Malawi jana katika Uwanja wa Bingu wa Mutharika jijini Lilongwe ilioshuhudiwa na Marais Samia Suluhu Hassan na Lazarus Chikwera. Timu hizo hazikufungana. **PICHA: MTANDAO**

# WAKONGWE SIMBA, YANGA WATAKA WACHEZAJI WAZAWA KUJITAMBUA

## ●●●Washangaa namna wageni wanavyopata fursa za kucheza nje huku wenyeji wakiendelea kubaki...

**Na Adam Fungamwango**

BAADHI ya wachezaji wa zamani wa klabu za Simba na Yanga wamewataka wachezaji wazawa kupambana na kujituma ili kuleta ushindani kwa wachezaji wa kigeni na kuacha kusubiri huduma ya wadau ya kutaka kutengenezewa kanuni rafiki zitakazowabeba mbele ya wageni.

Wakizungumza na gazeti hili, beki wa zamani wa Simba, Amri Said 'Stam' na winga wa Yanga, Sekilojo Chambua wote wamesema inasikitisha kuona wachezaji wazawa wakibweteka kwa majina yao na wakishuhudia wachezaji wa kigeni wakizifanya timu hizo ngazi ya mafanikio kwa kwenda kucheza soka nje ya Tanzania.

Walisema mchezaji anayesubiri kuwekewa kanuni rafiki kwa kupunguza wachezaji wa kigeni, au kulazimishwa waanze wazawa wengi hawezi kuiva na kukamilika kuwa bora kuichezea timu ya taifa na hata kwenda kucheza soka la kulipwa nje ya nchi.

Wakongwe hao wametoa ushauri huo baada ya kuona nafasi za wazawa zimekuwa finyu kwenye klabu kubwa za hapa nchini na hata nafasi za kwenda nje zikitokea ni wachezaji wa kigeni wanaochukuliwa.

"Wachezaji wazawa wazuri wapo, wana vipaji vya kutosha na wanaweza kufanya kazi kubwa vizuri tu na wanazo nafasi, ila inabidi wafanye kazi ya ziada, wajitoe kwa sababu wageni huwa wanajituma, wanapambana na kujitoa sana kwa sababu wana malengo, wanajitambua, wanakuja Tanzania kufuata ngazi ya kwenda juu zaidi," alisema Saidi.

Alisema sasa hivi klabu za Simba na

UKURASA. 23

# Hatima ya Mayele Yanga kujulikana Jumatatu

**Na Saada Akida**

HATIMA ya mshambuliaji wa Yanga, Fiston Mayele, kuendelea kuwamo kwenye kikosi cha timu hiyo au kuondoka itajulikana Jumatatu ijayo baada ya timu hiyo kurejea nchini kutoka Malawi.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Mayele alisema anawasubiri viongozi wa klabu hiyo ili kutoa msimamo wake juu ya wapi atacheza msimu ujao.

Kauli hiyo ya Mayele imekuja baada ya kukutana na viongozi wake kwa mara tatu katika vikao vya kujadiliana kuendelea kuwamo ndani ya timu hiyo kwa msimu ujao.

Inaelezwa katika vikao hivyo, Yanga wamefikia dau la kumlipa mshahara wa Sh. milioni 34 kwa mwezi kama atakubali kuwa sehemu ya kikosi hicho kwa msimu ujao.

Akizungumza na Nipashe jana, Mayele alisema hayuko sehemu ya kikosi cha wachezaji waliokwenda Malawi na anatarajia kukutana na viongozi wake Jumapili au Jumatatu timu itakaporejea kutoka nchini humo.

Alisema mpaka sasa amepata ofa tatu kutoka katika klabu za mataifa matatu ya Ubelgiji, Qatar na Saudi Arabia na wote wamempa ofa nzuri.

"Bado sijajua maana tuneshakutana na viongozi wa Yanga katika vikao vitatu na hatujaelewana, tunatarajia kukutana tena kati ya Jumapili au Jumatatu kwa ajili ya kuzungumza baada ya hapo tutajua nini kitatokea, aidha niendelee kuwapo Yanga au vinginevyo," alisema Mayele na kuongezea,

"Baada ya kujua hatima yangu ninaimani Yanga wataweka wazi, sijawaza mambo mengi kwa sababu hawa watu walionipa ofa wameniona nikiwa Yanga, natakiwa kutumia akili nyingi kufanya uamuzi sahihi," alisema Mayele.

UKURASA. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >